# Nipashe

Jumatano Desemba 11, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581887

www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

Nipashe digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0677 020 710 LIKE & FOLLOW US

epaper.ippmedia.com MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii www.ippmedia.com


UKURASA WA 4

**Bilioni** 100/- zapokewa Akaunti ya Mirathi



UKURASA WA 8

**Tume ya Haki:** Vilio visipuuzwe Uchaguzi wa Serikali za Mitaa



UKURASA WA 19

**Netanyahu** apandishwa kizimbani mashtaka ya ufisadi

UKURASA WA 22

**ALLISTER: AWATAKA ARNOLD, VAN DIJK KUBAKI LIVERPOOL**

## SIKU YA HAKI

# Ukwasi wa mawaziri, ma-RC wazua jambo

• **Ukimya** kwenye utekaji nao wanyooshewa kidole... *Ukurasa 2*



Sheikh Ponda Issa Ponda



Jenerali Ulimwengu



Dk. Hellen Kijo Bisimba



Askofu Emmaus Mwamakula

# Samia: Janabi jiandae nafasi ya Ndugulile

UKURASA 3



Rais Samia Suluhu Hassan akimwapisha Prof. Palamagamba Kabudi kuwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Ikulu ndogo ya Tunguu, Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Mbowe, Lissu wavunja ukimya

• **Meza** moja watoa msimamo uchaguzi... *Endelea Ukurasa 18*




**MICHEZO** **YANGA: TUTAKUFA NA TP MAZEMBE** UK.24 **MAONI,** UK.6

# Ukwasi wa mawaziri, ma-RC wazua jambo

Na Christina Mwakangale




Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Jaji mstaafu Mathew Mwaimu akizungumza wakati wa kufungua maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

UKWASI walionao baadhi ya mawaziri na wakuu wa mikoa na wilaya nchini umezua jambo: Watetezi wa haki za binadamu wamehoji walikopata ukwasi huo viongozi hao wa serikali.

Ni hoja iliyoibuliwa na watetezi hao jana jijini Dar es Salaam wakati wa mkutano wa tafakuri ya hali ya utetezi na uenezi wa haki za binadamu nchini kwa kipindi cha miaka 40 ya uwapo wa haki hiyo kikatiba.

Hao ni pamoja na Jenerali Ulimwengu, Askofu Emmaus Mwamakula, Shehe Ponda Issa Ponda, Mpale Mpoki, Tike Mwambipile, Hellen Kijo-Bisimba, Rugemeleza Nsala na Kaiza Buberwa.

Bila kutaja jina la waziri, mkuu wa mkoa na wilaya, Ulimwengu, mwandishi mkongwe mwenye taaluma ya sheria, aliwataka waandishi wa habari wenzake wampatie majibu kuhusu ulikopatikana ukwasi walionao baadhi ya mawaziri, wakuu wa mikoa na wilaya nchini.

"Ninyi waandishi wa habari, mmeshawahi kujiuliza mishahara ya viongozi -- mawaziri, wakuu wa mikoa na wilaya wanapata kiasi gani? Kile kipato chao halali! Masurufu anayopata yanayotokana na nini? Na akija madarakani, mali zake zinatokana na vyanzo gani? Au hii ni hela yetu ambayo ilipaswa kujenga barabara?

"Au tunataka kuona anakula kwa kamba yake? Inawezekana kabisa nchi inashindwa kufanya shughuli zake... Nimewapa kazi hii waandishi wa habari. Mkishindwa, basi ninyi siyo waandishi wa habari.

"Ninazungumza hivi, ninaomba mnisaidie vyombo vya habari, mimi nimeshastaafu," alisema Ulimwengu na kuibua kicheko ukumbini, huku akisisitiza ni umuhimu viongozi wa umma kutaja mali zao na kuwaruhusu waandishi wa habari kuona viapo vya kutangaza mali zao na kila mwaka waulizwe tena.

Watetezi hao pia walionesha wasiwasi wao juu ya matukio yanayowakumba, huku wakitaka falsafa ya 4R ya Rais Samia Suluhu Hassan kujengewa misingi ya kisheria ili itekelezeke.

Mratibu wa Taifa wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), Onesmo Olengurumwa, alisema falsafa hiyo ya Rais Samia ya Maridhiano, Ustahamilivu, Mageuzi na Kujenga Upya inaweza kuwa na nia njema ingawa changamoto ya utekelezaji wake iko katika mifumo na wanaomzunguka.

"Falsafa ya Rais Samia inaweza kuwa yenye nia njema, shida ikawa kwa wanaomzunguka. Tumebaini hawana nia njema. Rais ndiye anataja haki za binadamu mara nyingi zaidi, haachi kila akizungumza, shida ni mifumo. Suala la Ngorogoro tulilizungumza bila woga, hatimaye akaunda tume," alisema.

Olengurumwa alisema kuwa kwa miaka ya karibuni, kumekuwako woga wa utetezi na utekelezaji wa haki za binadamu kutokana na watetezi wengi, hasa wanazuoni, viongozi wa dini, wastaafu na waandishi wa habari kutokuwa thabiti kwenye utetezi, akitaja vikwazo kadhaa kama vile kukosa usalama wao.

"Awali wataalamu wa vyuo vikuu walielimisha na kutoa elimu, walionya. Ilichangia mabadiliko makubwa ya kisheria, yalianzia vyuo vikuu, waliona umuhimu wa utetezi wakiwa wadau wakuu.

"Lakini hali inazidi kubadilika kadri siku zinavyozidi kwenda. Leo hii hali imebadilika, imeshuka! Huwezi kukuta mijadala, watu wakichambua, ukosoaji katika vyuo vya kitaaluma.

"Unaweza ukaita mjadala pale Chuo Kikuu (UDSM), ukakuta wanaohudhuria siyo wanachuo, si wanafunzi! Hadhi ya chuo kikuu kuwa chemchemu ya mawazo imebadilika, kuna changamoto," alitadharisha.

Kuhusu utetezi wa haki za binadamu kwenye mhimili wa mahakama, Olengurumwa alisema kuwa awali ulitumika kueneza na kutetea haki hizo kutokana na mamlaka iliyonayo. Sasa umeshuka kutokana na uamuzi unaotolewa hautekelezwi, akitolea mfano suala la mgombea binafsi ambalo halijatekelezwa na Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 ambayo Rebecca Gyumi alishinda kesi kuhusu umri wa kuoa na kuolewa. Nalo halijatekelezwa.

Olengurumwa alitaja kundi lingine ni la viongozi wa dini ambao wao tangu historia na kwenye vitabu vya dini wamekuwa mstari wa mbele kwenye usawa wa binadamu pamoja na kuchangia huduma za kijamii kama vile ujenzi wa hospitali, shule na vyuo.

Alisema kuwa hivi sasa jamii na baadhi ya viongozi serikalini wanadhani utetezi wa haki kwa viongozi hao ni kukiuka miongozo ya kidini.

Olengurumwa alisema kwamba kundi la mawakili limekuwa na mchango mkubwa kwa miongo minne nchini, lakini eneo la kisheria hivi sasa limepwaya. Wanakumbana na changamoto, huku baadhi wanaofika mahakamani wakionekana wasumbufu, hata kujengewa chuki na baadhi ya watoa uamuzi.

"Mawakili wengi hawataki kujihusisha na haki za binadamu, ukiwa mtetezi unakuwa katika migogoro. Ulinzi ili ukamilike lazima kuwe na kundi kubwa la utetezi. Sehemu kubwa wanaotekwa ni wanaosemasema," alidai.

Wakili Olengurumwa alisema kwamba kundi lingine la utetezi wa umma lililorudi nyuma ni la wazee wastaafu ambao ni wananchi waandamizi, akisema wanasita kukemea, kuonya na wakikaa kimya kwa kujifungia na maarifa, uzoefu na familia zao.

"Huu ni uchoyo wa maarifa na hekima. Viongozi waliobaki wachache ndio wanasema. Tumemsikia Jaji Warioba, Butiku na wengine wanajitokeza kusema kusaidia watanzania," alisema Olengurumwa.

Alisema asasi za kiraia awali zilifanya kazi kwa nyakati ngumu na kusikika nchi nzima. Hakukuwa na teknolojia ya mawasiliano, lakini hivi sasa watetezi hao wamerudi nyuma kuusemea na kuutetea umma, hata kwenye masuala ya uchaguzi.

"Suala la utekaji limechagiza watetezi wa haki za binadamu kwa makundi yote - mawakili, waandishi wa habari kurudi nyuma. Kwa mwaka mmoja waliotekwa kwa takwimu zetu ni watu 47 ingawa Jeshi la Polisi wao wanatoa takwimu za watoto kupotea.

"Takwimu za watu wazima ni chache na wakitaja wanatamka watu wamepotea, si kutekwa! Wamebadili lugha. Tangu mwaka 2016, watu waliotekwa ni zaidi ya 250," alidai.

Pia alisema kwamba kundi la waandishi wa habari ambalo ni la utetezi kwenye haki za binadamu nalo limekwamishwa na sheria ambazo zinawawabana, kwa kuminya uhuru wa habari, huku hadhi ya sekta hiyo ikishuka.

"Waandishi wa habari wengi sasa ni habari za kusifiasifia, hiyo ni mbaya! Matukio mengi mnafumbia macho, ingawa ni hatari, ila kunahitajika mbinu za kujikomboa bila kubagua. Kwa watetezi hawa karibu wote niliowataja, kunahitaja uhuru wa kiuchumi ili kutimiza majukumu ambayo ndio utetezi wenyewe," alieleza Olengurumwa.

**SIMBA NA YANGA**

Naye Ulimwengu alisema licha ya kuwapo mambo ya msingi ya kujenga hoja za kuikwamua nchi, vyombo vya habari nchini vimejawa mijadala inayoegemea burudani na michezo, hasa soka, wakizungumzia zaidi mwenendo wa timu za Simba na Yanga.

Alisema mijadala hiyo ingekuwa na uzito iwapo hata soka la taifa lingekuwa linafanya vyema, kitaifa na kimataifa, hivyo vyombo vya habari, hasa vya umma, viweke kipaumbele katika kujenga hoja za msingi, ikiwamo utetezi wa haki za binadamu.

"Yaani katika vyombo vya habari vya umma, binafsi kumejawa na 'usimba na uyanga kutwa nzima'. Wajibu wa waandishi wa habari uko wapi? Sisemi ni mbaya, ila isivyo bahati, hata huo mpira wenyewe hatuujui," alionya.

Naye Askofu Mwamakula alisema jamii inatakiwa kubadili dhana kwamba viongozi wa dini ni watetezi wa haki za binadamu, hivyo wanapokuwa mstari wa mbele kuzitetea, wasione ni ukiukwaji miongozo ya dini.

"Kama unafuata amri 10 za Mungu, ujue wewe ni mtetezi wa haki za binadamu. Ilipoanza serikali kuminya haki za kisiasa na viongozi wa dini wakaanza kutetea, ikaanza kuonekana wanapingana na serikali. Changamoto zikaanza katika mazingira hayo, wako wanaotishiwa kufutiwa usajili," alidai Askofu Mwamakula.

Mwanaharakati wa Haki za Binadamu, Helen Kijo-Bisimba, alisema utetezi wa haki za binadamu nchini umeendelea kuzorota, hasa kwa asasi za kiraia, jambo linalochangia kutoimarika kwa utetezi huo.

Naye Shehe Ponda alikosoa Sheria ya Ugaidi kwamba ina vifungu vinavyomruhusu askari kumhoji na kumtesa mshtakiwa/ mtuhumiwa, akisema hatua hiyo inarudisha nyuma utetezi wa haki za binadamu. Mtu anaadhibiwa hata kabla hayajapatikana na hatia.

Wakili Dk. Nshala alisema kwamba hivi sasa wanazuoni wamepungua nguvu ya utetezi wa haki za binadamu kwa kuwa walio wengi wanaangalia maslahi binafsi, ikizingatiwa mtoa ajira wa kundi hilo vyuoni ni serikali, hivyo utoaji hoja unaokosoa serikali huwa ni mgumu kwao.

***Kwa maoni kuhusu habari hii: Piga/sms / WhatsApp : +255 677 020 701***

HABARI KITAIFA

# Samia: Janabi jiandae nafasi ya Ndugulile

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS Samia Suluhu Hassan, jana amewaapisha mawaziri, manaibu waziri, makatibu wakuu na mabalozi, aliowateua hivi karibuni huku akimtaka Profesa Mohamed Janabi aliyemteua kuwa mshauri wa Rais katika masuala ya afya, kujiandaa kugombea nafasi iliyoachwa wazi na Hayati Faustine Ndugulie ya Ukurugenzi wa Shirika la Afya Duniani (WHO) kanda ya Afrika.

Ndugulile aliyekuwa mtaalamu wa afya ya umma na Mbunge wa Jimbo la Kigamboni, alikuwa mmoja wa wagombea watano waliojitokeza kumrithi Dk. Matshidiso Moeti, raia wa Botswana.

Alipaswa kuapishwa Februari 2025, lakini umauti ulimchukua kabla ya kukalia kiti chake.

Akiwaapisha wateule hao Ikulu ya Tunguu, Zanzibar, Rais Samia alisema, kutokana na wadhifa wa Profesa Janabi, jina lake limependekezwa na kupelekwa katika mchakato wa kugombea nafasi hiyo.

Akizungumza na viongozi hao baada ya kuwaapisha, hafla iliyohudhuriwa na viongozi mbalimbali akiwamo Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais Samia alisema kutokana na kasi ya ukuaji wa sekta ya mawasiliano na teknolojia ya habari duniani, serikali imekuja na mkakati wa kidijitali wa kitaifa unaohitaji kushughulikiwa ipasavyo.

Alisema bado hajaridhishwa na kasi ya utendaji katika teknolojia ya habari na ni lazima kwenda na kasi katika hiyo, ndio maana ameitoa sekta ya habari katika Wizara ya Mawasiliano na kuipeleka katika Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Pia, mawasiliano ndani ya nchi na kuunganisha nje ya nchi ikiwamo minara ya simu ambayo inahitaji kazi kubwa ya kulifanya Shirika la Simu (TTCL) na Shirika la Posta kusimama yenyewe na kuwa kibiashara.

Alisema kubadilisha nafasi za mawaziri na manaibu waziri kutoka wizara moja kwenda nyingine lengo lake ni kuongeza ufanisi ndani ya serikali.

Aliwataka viongozi hao aliowaapisha kwenda kufanya kazi vizuri kwa kushirikiana na watendaji wengine katika wizara husika ili kuliletea maendeleo taifa katika kila nyanja.

Alisema amemteua Profesa Palamagamba Kabudi kuwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo baada ya kupitia wasifu wake, pia ni mwanahabari na ana uzoefu mkubwa unaompa imani kuwa atafanyakazi vizuri katika sekta hiyo.

"Nenda kaikamate vizuri sekta ya habari unajua vizuri changamoto zilizopo pamoja na changamoto za wanahabari," alisema Dk. Samia.

Kuhusu uteuzi wa Dk. Ashantu Kijaji kuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, alisema amekuwa akimhamisha kutoka wizara moja kwenda nyingine na sasa ni wakati wa kuvaa suruali ya jinzi na kutoka ofisini kwenda kwa wafugaji na wavuvi kufanya kazi kwa sababu kuna kero nyingi za wafugaji kuingia katika hifadhi pamoja na mashamba ya wakulima.

Aidha alimtaka Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Hamad Yussuf Masauni, kuimarisha Muungano ili kujijengea wadhifa mzuri wa kuendelea kubaki katika Jimbo la Kikwajuni kwa sababu linazingirwa katika nafasi ya ubunge.

Akizungumzia kuhusu nafasi za ubalozi, Rais Samia alisema aliowateua hasa wa upande wa kisiasa wanaowakilisha Tanzania katika nchi mbalimbali ni ambao bado wanafanya vizuri na wapo ngangari kwa sababu baadhi ya mabalozi wamefika umri wa kustaafu na anawerejesha nchini kuunga mkono katika kampeni za uchaguzi mkuu.

Aliwataka mabalozi hao kuwa ngangari kwa sababu baadhi ya maeneo wanayokwenda kufanya kazi kuiwakilisha Tanzania hayapo tulivu na amefanya uteuzi wa mabalozi kwa kutumia vigezo ikiwamo vya uaskari.

"Tunataka mkaweke nguvu kwa sababu baadhi ya maeneo mnayokwenda sio salama kwa mfano Msumbiji na maeneo mengine na ndio maana baadhi ya mabalozi tumeachagua wapo katika kazi ya uaskari," alisema.

Naye Makamu wa Rais aliwasihi viongozi hao, kwenda kufanya kazi kwa ushirikiano na viongozi wengine na kuheshimu mawazo ya wataalamu waliowakuta katika nafasi zao ili kuwaletea ushindi wananchi wa Tanzania kwa maisha bora zaidi.

Aliwataka mabalozi walioapishwa kwenda kufanya vyema kwenye diplomasia ya uchumi ili jitihada za Rais Samia kupitia falfasa ya 4R itekelezwe kikamilifu.

Alisema viongozi hao wana kazi kubwa ya kuhakikisha wanayoyataka Watanzania yanatekelezwa kikamilifu kuendana na Ilani ya CCM na watakapoingia katika Uchaguzi Mkuu wa 2025 wanafanya kazi ambayo Rais na Watanzania wote wanaitarajia.

***Kwa maoni kuhusu habari hii:***
***Piga/sms / WhatsApp : +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@guardian.co.tz***


Nipashe
WhatsApp Chaneli
Skani hapa kutembelea chaneli yetu



The Guardian Limited

**VACANCY**

**Sales Freelancers**

**The Guardian Limited** is looking for self driven sales Freelancer to join our **advertising** Sales Team in **Dar es Salaam, ( Moshi, Arusha, Tanga, Morogoro, Iringa, Mwanza and Zanzibar)**

**Responsibilities**

- Be responsible for aggressive development of new clients and growing existing business.
- Proactively develop new business avenues
- Devise and monitor business plans to ensure substantive sales
- Develop strategic solutions that meet the unique needs of each client

**Qualifications**

- The position requires someone who can deliver the set targets within deadlines under competitive working environment.
- Applicants need to be highly organized, self-motivated with a positive attitude, and can thrive on setting and reaching new goals.
- Holders of a University degree or Diploma in Business Administration
- Experience in Sales and Marketing is an added advantage

**NOTE: This is a commission Based Position**

182777

**Please send your application via Email to vacancy@guardian.co.tz before 15st December, 2024.**



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

**TANGAZO LA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MIKOA YA ARUSHA, KILIMANJARO NA DODOMA KATIKA HALMASHAURI ZA WILAYA ZA CHEMBA, KONDOA NA MJI WA KONDOA**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza unafanyika katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Dodoma katika Halmashauri za Wilaya za Chemba, Kondoa, na Mji wa Kondoa kuanzia tarehe 11 hadi 17 Desemba, 2024. Zoezi la uboreshaji wa Daftari linafanyika kwa siku saba kwa kila kituo katika Mikoa hiyo.

1. SIKU: Uboreshaji unaanza siku ya Jumatano tarehe 11 hadi Jumanne tarehe 17 Desemba, 2024.
2. VITUO: Uboreshaji unafanyika katika vituo vilivyopo kwenye Mitaa, vijiji na vitongoji.
3. MUDA: Vituo vinafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni.

**Uboreshaji unahusisha: -**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa Miaka 18 na zaidi na hawakuwahi kuandikishwa hapo awali.
2. Kuandikisha Wapiga kura ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.
3. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi
4. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
5. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
6. Aidha,Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume www.inec.go.tz au anuani ya ovrs.inec.go.tz kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la kata kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo watakwenda nayo kituo cha kujiandikisha ili kukamilisha taratibu na kupata kadi ya mpiga kura.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni.
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo.
- Mpiga Kura ambaye ana simu ndogo maarufu kama kitochi au kiswaswadu anaweza kuingia kwenye mfumo huo kwa kupiga *152*00#. Kisha, atachagua Namba 8 na kubonyeza, baada ya hapo atachagua namba 2 na kubonyeza, Kisha atachagua namba 3 (Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi) na hapo, atapata huduma namba moja hadi nne. Atachagua huduma anayoitaka kati ya hizo nne. Hatimaye, atapata namba ya utambulisho (token number) atakayokwenda nayo kituoni kukamilisha mchakato wa kupata kadi ya mpiga kura.
- Mpiga kura anaweza pia kuwasiliana moja kwa moja na Maafisa wa Tume waliopo katika Kituo cha Huduma kwa Mpiga Kura kwa kupiga namba 0800112100 bila malipo.
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao waliandikishwa awali, hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

**KUJIANDIKISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA**

Limetolewa tarehe 03 Desemba, 2024 na:

**Livini A. Morrice**
**KAIMU MKURUGENZI WA UCHAGUZI**

218284201



Mafundi wa kampuni ya ujenzi ya mkandarasi, wakiendelea na ujenzi wa Kituo cha mabasi yaendayo haraka cha Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mahakama yatoa maelekezo ya mwisho kesi ya wanandoa

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam imewapa maelekezo wanandoa Bharat Nathwan (57) na Sangita Bharat (54) wanaotuhumiwa kwa kesi ya kujeruhi na kutoa lugha ya matusi kwamba Januari 7,2025 kama wakili wao hatakuwapo mahakamani, kesi itaendelea kusikilizwa pasi na kuwapo kwake.

Imeeleza kwamba haitaki kuamini kwamba Wakili wa Utetezi Gabriel Mnyele, ambaye ni wakili mkongwe, hajafika mahakamani bila sababu ya msingi, hivyo inampa nafasi nyingine kutekeleza wajibu wake.

Hayo yalisemwa jana na Hakimu Mkazi Mkuu Aaron Lyamuya wa mahakama hiyo baada ya Wakili wa Utetezi, Edward Chuwa kuomba busara ya mahakama kutokuendelea na usikilizwaji shauri hilo kwa kuwa wameandika barua Mahakama Kuu.

Baada ya kudai hayo, Wakili wa Serikali Faraji Ngukah alidai kuwa wana shahidi mmoja na wako tayari kuendelea na kuhusu barua hiyo, alidai hawajapata nakala, pia haizuii kuendelea na chochote.

"Nimemsikia Wakili Chuwa, ni haki yao kuomba, lakini hatujapokea nakala ya barua. Na hata kama hatujapokea haizuii kuendelea na chochote kwa sababu hakuna sheria inayoelekeza lazima wapewe," alidai Wakili Ngukah.

Pia alidai kuwa waendelee na usikilizwaji, siku Mahakama Kuu ikitokea ikazuia basi kesi itasimama. Haijulikani barua itajibiwa lini na shahidi huyo amemtoa sehemu muhimu, amefika mahakamani kutoa ushahidi.

Hakimu Lyamuya baada ya kusikiliza hoja zao, alisema kesi hiyo imekuwa na mambo mengi, ndio maana ameamua kuihamishia chumba cha wazi cha mahakama kwa ajili ya watazamaji, ili nao wahukumu anasikiliza kesi vizuri au vibaya.

"Imeeleza kwamba mmeandika barua kwa Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu, utaratibu ni kwamba unapotaka kufanya jambo huko, unafanya maombi rasmi na si barua. Inaweza ikasomwa na isifanye chochote," alisema Hakimu Lyamuya.

Alisema barua haiwezi kuihamisha mahakama, jaji akitaka mwenendo wa kesi anaangalia moja kwa moja kwa kuwa kila kitu kimo katika mtandao, kila kitu anakiona.

"Hadi hivi sasa sioni chochote hapa, mnachosubiri ninyi ni kudra zake tu, hamjui ni lini hiyo barua kujibiwa. Nisingeahirisha kesi kwa sababu hii mwenendo wa kesi ungekuwa batili, Mnyele hayupo mara ya pili, nampa nafasi nyingine," alisema.

Hakimu Lyamuya alisema anaahirisha kesi hiyo kwa sababu Mnyele hakuwa mahakamani na washtakiwa wana haki ya kuwa na uwakilishi na pia katika utendaji kazi wake hajawahi kuona barua imeandikwa kesi ikaahirishwa.

Wakili Ngukah alidai hana pingamizi na uamuzi wa kiti, lakini walitaka Chuwa awaeleze alikokuwa Mnyele. Hakimu Lyamuya aliwaeleza kwamba kila mtu na haki ya kupewa nafasi nyingine, hivyo ametoa kwa wakili huyo.

"Ninatoa maelekezo kwa washtakiwa, ninaomba mnisikilize kwa makini, ninyi mmeweka mawakili Januari 7, 2025. Kama wakili wenu hatakuja, tutaendelea bila yeye kuwapo, zingatieni sana ninyi ni washtakiwa, hakuna wengine, ni ninyi," alisema.

Wanandoa hao ambao ni raia wa Tanzania wenye asili ya India wanaoishi Mtaa wa Mrima - Kisutu, jengo la Lohana Dar es Salaam, washtakiwa kwa mashtaka manne wanayodaiwa kuyatenda Julai 21, 2023 kinyume cha sheria.

Ilidaiwa kuwa Nathwan anatuhumiwa Julai 21, 2023, akiwa eneo la mtaa wa Mrima-Kisutu, jengo la Lohana, ndani ya Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam kinyume cha sheria. Wanadaiwa walimsababishia madhara makubwa Kiran Lalit kwa kuzamisha kichwa chake katika ndoo ya saruji iliyochanganywa.

***Kwa maoni: +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@guardian.co.tz***


Victoria FINANCE

Victoria Finance Plc
5th Floor, Mwanga Tower Building-Kijitonyama
New Bagamoyo Road
P.O. Box 12102, Dar es Salaam - Tanzania

Telephone +255 22 277 4577
Fax: +255 22 277 4559
Email: info@victoriafinance.co.tz
Website: www.victoriafinance.co.tz

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

VICTORIA FINANCE PLC INAPENDA KUUTANGAZIA UMMA YA KWAMBA KWA IDHINI ITAKAYOTOA KWA KAMPUNI TOFAUTI ZA UDALALI INATARAJIA KUUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU KAMA IFUATAVYO;

| NA. | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | NYARAKA YA UMILIKI NA SEHEMU | DALALI | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | *SHAMIMU HABIBU KAHUNGU T/A LAWRENCE TENDAYI RUSERE* | *GARI* | *T125 EDG - VOLKSWAGEN TIGUAN* | *JODAC PROFESSIONAL LTD* | *17/12/2024* |
| 2 | *INTERCON TRADING COMPANY (T) LIMITED* | *GARI* | *T170 EEM -BMW X3* | *GSP AUCTION MART* | *20/12/2024* |

Minada yote itafanyika mahali husika katika muda na siku ambayo itatangazwa kupitia katika vipeperushi na magari ya matangazo kutokana na idhini itayotoka kutoka katika vyombo husika vya Serikali.

**MASHARTI YA MNADA;**

- Asilimia 25% ya bei iliyofikia italipwa papo hapo na asilimia 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne. (14). Kwa kushindwa kufanya hivyo itapelekea mnada kurudiwa tena na pesa zilizolipwa kutokurudishwa.
- Gharama za kumuhamisha mmiliki na kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.
- Dhamana itauzwa Kama ilivyo.

***218293001***


# Zaidi bil. 101/- zapokewa katika akaunti ya mirathi

**Na Kulwa Mzee**

JAJI Mkuu wa Tanzania, Profesa Ibrahim Juma, amesema katika miaka mitatu tangu kuanzishwa kwa Kituo Jumuishi cha Masuala ya Familia Temeke, jumla Sh. bilioni 101.8 zilipokewa katika akaunti ya mirathi.

Kati yake, Sh. bilioni 77.8 zililipwa kwa warithi na Sh. bilioni 24 zinasubiri kulipwa.

Jaji Ibrahim alisema hayo jana wakati wa kilele cha maadhimisho ya miaka mitatu ya Kituo Jumuishi cha Masuala ya Familia Temeke tangu kuanzishwa mwaka 2021.

Alisema mirathi hubeba kiasi kikubwa cha fedha na uendeshaji wake unahitaji umakini na uadilifu wa hali ya juu vinginevyo inaweza kugubikwa na ubadhirifu.

Jaji Profesa Ibrahim alisema wakati wa kutayarisha Mpango Mkakati wa Mahakama na Programu ya Maboresho miaka ya 2014 hadi 2016, Mahakama ya Tanzania ilikuwa ikikabiliana na changamoto ya usimamizi wa fedha na mali za mirathi.

Alisema kupitia mashauri ya mirathi Mahakama ilikuwa inalipa Sh. bilioni 3.8 kwa wasimamizi na warithi wa mirathi kiasi ambacho kinabeba uchumi mkubwa wa wananchi mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

"Mahakama iliona ni muda mwafaka wa kuimarisha na kuboresha ushughulikiaji na usimamizi wa mashauri ya mirathi kwa kuyapa kipaumbele ili kuhakikisha wananchi na jamii kwa ujumla wanapata huduma na elimu ya usimamizi wa mirathi na utatuzi wa migogoro ya kifamilia ili kutumia muda wao zaidi katika shughuli za kiuchumi na kimaendeleo.

"Katika miaka ya Fedha 2021/2022, 2022/2023, 2022/2024 na 2024/2025 jumla Sh. 101,876,509,671.81 zilipokewa kwenye akaunti ya mirathi, kati ya hizo jumla ya Sh. 77,846,349,370.59 zililipwa kwa warithi na jumla ya Sh. 24,030,169,397 zinasubiri kulipwa.

"Ipo changamoto kubwa ya baadhi ya wasimamizi wa mirathi kukiuka masharti ya kisheria juu ya majukumu yao ya usimamizi wa mirathi, baadhi ya wasimamizi hawaziishi ahadi walizoapishwa mahakamani," alisema Jaji Mkuu.

Alisema takwimu zinaonesha kuwa hadi sasa, Kituo Jumuishi kimewahudumia wateja 580,610, kati ya hao 311,183 ni wanawake, 265,985 wanaume na 3,442 watoto.

Alitaja faida zilizopatikana katika kipindi cha miaka mitatu kuwa gharama zimepungua kwa wananchi na wadaiwa katika kufuatilia huduma za haki ambazo zinatolewa na wadau tofauti katika sehemu tofauti kwa kuwa utoaji wa huduma jumuishi unarahisisha huduma hizo kupatikana katika jengo moja.

"Kituo Jumuishi cha Masuala ya familia Temeke, kimebeba dhana ya maboresho kwa kuwa na mfumo wa utoaji haki ambao unalenga kuwafikishia huduma wananchi ambao ni wanyonge katika jamii na ambao huduma za kimahakama huwa haziwafikii kwa wepesi na kwa gharama nafuu.

"Walengwa hapa ni wale katika jamii ambao huwa hawapati nafasi sawa na wengine katika kupata huduma za utoaji haki kwa mfano, wanawake, watoto, watu wenye ulemavu na wanaoishi katika mazingira magumu, wametajwa kuwa hawapati fursa sawa na wengine katika kufikia ngazi za utoaji haki," alisema.

Alisema katika kuhakikisha wananchi wenye kipato cha chini Dar es Salaam wanapata usafiri wa kuwafikisha katika Kituo Jumuishi Temeke, Andiko la Mradi wa Maboresho ya Mahakama iliitaka Mahakama ya Tanzania ifanye makubaliano na uongozi unaosimamia Mabasi ya Mwendokasi ili kuweka punguzo la nauli za mabasi yao kurahisisha usafiri wa wadaiwa wanaofuata huduma katika Kituo Jumuishi.

Jaji Mfawidhi wa Kituo Jumuishi cha Masuala ya Familia Temeke, Mwanabaraka Mnyukwa alisema: "Katika kipindi cha miaka mitatu tumekutana na changamoto ya ucheleweshaji wa kuhamisha mali kwenda kwa warithi, jamii kutokuwa na uelewa kuhusu usimamizi wa mitathi.

"Mahusiano wanandoa katika kuvunja ndoa na uelewa mdogo kuhusu kuandika wosia, kuandika wosia ifahamike kwamba si uchuro," alisema Jaji Mwanabaraka.

"Wanandoa wamekuwa na uadui, wanatakiwa kuwa na makubaliano katika haki ya kuwaona watoto na mgawanyo wa mali," alisema.

Alisema Kituo kimehudumia idadi kubwa kwa miaka mitatu jumla ya watu 580,610 walihudumiwa wakiwamo wanawake 266,985, wanaume 311,183 na watoto 3442.

Jaji Mwanabaraka alisema jumla ya mashauri 22,929 yalisajiliwa kati ya hayo yaliyoamuliwa ni 20,077 na 852 hadi Agosti, mwaka huu yalikuwa hajasikilizwa.

Alisema migogoro inasababisha chuki kwa wanafamilia na kusababisha warithi kuchelewa kupata haki zao kwa wakati.

## HABARI PICHA

# BALOZI WA JAMHURI YA KOREA KUSINI EUNJU AHN ATEMBELEA THE GUARDIAN LTD



Mhariri Mtendaji wa Gazeti la The Guardian, Wallace Mauggo, akitoa maelezo kwa Balozi wa Jamhuri ya Korea Kusini, Eunju Ahn (katikati), alipotembelea chumba cha habari cha Kampuni ya The Guardian Ltd (TGL) inayochapicha magazeti ya The Guardian na Nipashe, Mikocheni, Dar es Salaam jana. Kushoto ni Naibu Meneja Mkuu wa TGL, Jackson Paulo, Meneja wa Fedha wa TGL, Samweli Orgeness (wa pili kulia) na wakuu wa idara mbalimbali. **PICHA ZOTE: MIRAJI MSALA**



Balozi wa Jamhuri ya Korea Kusini, Eunju Ahn (katikati), akifurahia jambo na viongozi wa TGL.



Mhariri wa Habari wa gazeti la Nipashe na Mkuu wa Kitengo cha Dijitali, Salome Kitomari (kulia), akitoa maelezo kwa Balozi Eunju Ahn, alipotembelea kitengo hicho.



Balozi Eunju Ahn, akiangalia mchoro wa sura yake uliochorwa na Mchora Katuni wa TGL, Muhidini Msamba (kulia).



Balozi Eunju Ahn, akisalimiana na Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe. Katikati ni Mhariri Mtendaji wa gazeti la The Guardian, Wallace Mauggo.



Balozi Eunju Ahn akipata maelezo kuhusu uchapishaji wa magazeti ya TGL kutoka kwa Meneja wa Kiwanda cha Uchapishaji cha TGL, Balasubramaniyan Venkadachalam (kushoto). Kulia ni Naibu Meneja Mkuu wa TGL, Jackson Paulo.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kuongezeka matukio utekaji, mauaji nini kinasababisha

**KURIPOTIWA** kwa matukio ya utekaji na mauaji ya mara kwa mara katika maeneo mbalimbali nchini kunaleta maswali mengi yanayokosa majibu.

Hapa nchini matukio hayo yalizoeleka kusikika katika nchi nyingine na kuonekana kama sinema kwa sababu Tanzania ni nchi inayosifika duniani kuwa ni ya amani na utulivu ndio sababu wageni wengi wanamiminika kuja kuitembelea na kuangalia vivutio vya utalii.

Utekaji na matukio ulioanza kujitokeza kwa sasa unaleta hali ya wasiwasi na kusababisha wananchi kuishi kwa wasiwasi kwa sababu hawajui lini yatawakuta.

Hali hii inasababisha hata baadhi ya watu kuhofia kufanya shughuli za maendeleo kwa kuwa hawafahamu wakati gani wanaweza kupatwa na mkasa.

Kuibuka kwa matukio haya kumesababisha watu kunyoosheana vidole bila kujua kiini cha tatizo hilo ni nini.

Takribani miaka mitatu iliyopita kuliibuka matukio ya watu kutoweka wakiwamo waandishi wa habari na wengine mpaka leo hawajulikani walipo.

Hali ilirudi kuwa shwari, lakini sasa imeanza kuibuka tena na kwenye jamii yamepamba moto kutokana na taarifa zinazoripotiwa kila mara matukio hayo kufanyika.

Kinachosikitisha zaidi hata watoto wasiokuwa na hatia wameingizwa kwenye matukio hayo na kupotezewa maisha yao.

Matukio ya hivi karibuni yameonesha majaribio ya watu kutekwa, wengine kuuawa kwa kudhania kuwa ni watekaji na tukio lingine ni la mfamasia aliyeuawa na kisha mwili wake kukutwa ukiwa umefukiwa karibu na nyumba yake.

Vitendo hivi vinasikitisha na sasa imeonekana ni kama wimbi linalovuma la utekaji na mauaji.

Kwa hivi karibuni Mkoa wa Dodoma, kumeripotiwa matukio kadhaa ya kinyama na mauaji na watu kuhoji kuna upepo gani mbaya umeikumba nchi yetu.

Wanaotekeleza unyama huo haifahamiki kama wanafanya kwa kulipiza kisasi au kwa sababu za kishirikina.

Huku Jeshi la Polisi likifanya uchunguzi kuhusu matukio hayo, inasikitisha kuona vikiendelea kufanyika na wanaofanya vitendo hivyo bado ni watu wasiojulikana.

Watu kutekwa, kutoweka na kuondolewa uhai sasa zimekuwa taarifa zinazotawala vyombo vya habari pamoja na mitandao ya kijamii.

Matukio haya yalianza taratibu, lakini yanakoendelea yanaweza kuwa makubwa na kusababisha wananchi kuhofia kutembea kwa amani kwenye nchi yao.

Jeshi la Polisi linafanya uchunguzi kuhusu matukio hayo na imani ya wananchi kuwa waliofanya vitendo hivyo vya kinyama watakamatwa ili sheria ichukue mkondo wake.

Damu za watu haziwezi kupotea bure, hata kama waliofanya vitendo hivyo watakuwa wamekimbia kwenda maeneo ya mbali, lazima watajulikana.

Wananchi pia ni lazima tutoe ushirikiano kulisaidia Jeshi la Polisi kuwapata wahalifu hao ili nchi yetu isiingie doa.

Sisi sote ni walinzi na tunapotoa ushirikiano kazi ya kupatikana kwa wahalifu hao itakuwa rahisi. Hakuna anayependa kuona uhai wa mtu ukiondolewa kwa sababu za chuki na ubinafsi au ushirikina.

Tanzania ni nchi ya kisiwa cha amani na amani hii iendelee kudumishwa ili tuendelee kupokea wageni wanaokuja kujifunza kwetu jinsi ya kuishi kwa umoja na upendo.

Viongozi wa dini ni watu wanaoaminika na waumini wao, wanapoongea ni sawa na kutoa ujumbe kutoka kwa Mungu. Hivyo ni jukumu lenu kuhakikisha watu wanarudi katika hofu ya Mungu na kuepuka vitendo vya kinyama.

**Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki Afrika.**

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Mwandishi Wetu

# Miaka 63 imelinda wanawake kiafya

**KATIKA** kusherehekea miaka 63 ya uhuru wa Tanganyika ambayo leo ni Tanzania Bara, wanawake wana mengi ya kujivunia mojawapo ni kupungua idadi ya vifo vya wazazi na watoto.

Kwa miaka mingi idadi ilikuwa kinamama 556 kwa kila vizazi hai 100,000 waliopoteza maisha.

Ni tatizo lilikuwapo kuanzia mwaka 2016 lakini juhudi zaidi zimefanyika na sasa vifo vimepungua hadi 104 mwaka huu.

Hata hivyo, wanawake wanaozaa raia wa taifa hili kuanzia wapigakura, walipakodi, wahandisi na viongozi wa kada zote wanalalamika kwanini wapoteze maisha kwenye uzazi?

Wanataka asife hata mmoja kwenye uzazi hasa kwenye changamoto ambazo zinaweza kuzuilika.

Kadhalika mafanikio mengine ambayo pia ni kupunguza vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano ambao nao idadi ya wanaopoteza maisha imepungua kutoka 67 kwa kila vizazi hai 1,000 hadi vifo 43 ni juhudi za kulinda uhai.

Lakini, kwani hata hao wapotee? Ni lazima juhudi zaidi zifanyike asife hata mmoja kwa sababu zinazoweza kuzuilika.

Serikali imeongeza ujenzi na kuboresha miundombinu ya huduma za afya kwa wazazi ni jambo jema linalostahili kusifiwa lakini kazi bado.

Nchi ikielekea kwenye miaka 64 ya uhuru idhibiti watoto wetu wasichana kulazimishwa kuwa mama katika umri mdogo kwa kuozwa na wanafamilia zao au kupewa mimba utotoni.

Zama hizi utaalamu upo tena wa kielektroniki wanaolaghai kuoza na kunajisi watoto hadi kupata mimba na kukatizwa masomo huku wakibebeshwa mzigo mzito wa kuwalea wamulikwe.

Ikumbuke pamoja na adha za mimba na ndoa utotoni, mwezi huu tunapoendelea na siku 16 za kuhamasisha umma kupinga ukatili wa kijinsia, tuone sote kuwa haipendezi watoto wenye miaka 14 au 13 wakiajiriwa majumbani.

Ni sheria ya kazi na mahusiano kazini ya mwaka 2004 inayoruhusu mtoto kuajiriwa ili kupata kipato.

Lakini, tujiulize ni nani anayejua hali ya mtoto huyo huko mijini anakofanyakazi?

Anatumikishwa kazi ngumu, hasomi wala hawezi kujitetea, hebu tumjali mtoto huyo kwa kukataza ajira ya watoto kwa namna yoyote ile wawe madarasani.

Sheria nyingine ambayo si rafiki wa mtoto ni ile ya ndoa ya mwaka 1971, bunge, wanaharakati, wizara na wanasheria pamoja na mahakama fuatilieni irekebishwe.

Hivi kuna haja ya watoto kuendelea kuoza wasichana au mabinti wa miaka 13 au 14 katika dunia ya sasa.

Serikali inapowezesha kupatikana huduma za kibingwa na bobezi kwa gharama nafuu kwenye hospitali za umma na kuwajali wanawake, wazazi, watoto wao isisahau kukomesha mambo yanayochangia vifo vya wazazi na watoto kwenye ujauzito ambako umri mdogo nao unahusika.

Ustawi wa vizazi vya sasa na vijavyo ni muhimu kuchochea kukua na uchumi afya bora, ustawi na maendeleo kwa kila mmoja.

Katika kuwa na taifa bora yote ni muhimu lakini kuandaa wanawake na watoto bora wa kizazi kijacho ni muhimu zaidi.

Hawa wataandaliwa kwa kuboresha sekta zote mtambuka kuanzia ya afya, elimu, teknolojia, kilimo ili kupata chakula, usalama, sheria na ulinzi.

Ni kazi njema ya kusambaza dawa, vifaa tiba na chanjo kwa watoto, lakini kama hawatalindwa dhidi ya unyanyasaji kingono, utoro shuleni, udumavu, utumikishwaji majumbani, dhuluma za kuozwa utotoni, kukeketwa itakuwa ngumu kuwa na vizazi vya sasa vilivyolindwa ili kupata Tanzania bora ya kesho.

HABARI KITAIFA

## Wakulima walia kuchelewa kusambazwa mbolea, mbegu

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

WAJUMBE wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Tanzania (ALAT) Mkoa wa Singida, wamelalamikia kuchelewesha kwa usambazaji mbolea na mbegu huku msimu ukiwa umeshaanza jambo ambalo litasababisha wakulima kutopata mavuno mengi.

Walitoa malalamiko hayo juzi, wakati wa kikao cha ALAT Mkoa wa Singida kilichofanyika wilayani Ikungi.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida, Elia Digha, alisema katika Mkoa wa Singida, msimu wa mvua unaisha Aprili na kitendo cha kumcheleweshea mkulima mbegu na mbolea za ruzuku ni kutomtendea haki na kusababisha asipate mavuno ya kutosha.

"Ifike mahali tuwatendee wakulima haki zao, mbegu na mbolea za ruzuku ziletwe kati ya Septemba na Oktoba kila mwaka na kuanza kusambazwa kwa wakulima kabla ya msimu wa kilimo haujaanza, sasa kuleta pembejeo hizo wakati msimu umeshaanza hakuna maana," alisema.

Mjumbe wa ALAT, Zainab Kihara, alisema hata mbegu na mbolea zinapofika wakulima wamekuwa wakipata changamoto ambapo mkulima anakuwa na kadi ya kupata pembejeo, lakini kunakuwa hakuna namba yake ya simu na kucheleweshewa kupata pembejeo.

Mwenyekiti wa ALAT Mkoa wa Singida, Moses Mkwega, alisema chanzo kikubwa cha mapato kwa mkoa huo ni kilimo na kwamba uwekezaji mkubwa usipofanyika katika sekta hiyo mapato kwenye halmashauri yatashuka.

Mkwega aliwaomba wajumbe wa ALAT kwenda kusimamia kilimo katika halmashauri zao na kuhakikisha wakulima wanapata mbolea na mbegu kwa wakati ili kuongeza mavuno.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, Asia Messos, alisema katika halmashauri yake wamekuwa wakiwahamasisha wakulima kwa kuwafikia vijiji kwenda kuchukua mbegu na mbolea za ruzuku na katika msimu wa kilimo hakuna mkulima atakayekosa pembejeo.

Naye Mkulima Omary Mbawa alisema maeneo mengine unakuta bango limewekwa kwamba eneo hilo kuna wakala wa mbegu na mbolea za ruzuku, lakini wakulima wakifika hawapati huduma jambo ambalo aliiomba serikali kusaidia kufanyanuchunguzi katila maeneo yote yaliyoainishwa kuwa ni ya mawakala.

Hivi karibu Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, alitoa wiki mbili kwa wakuu wa Idara ya Kilimo mkoani hapa ifikapo Disemba 15, mwaka huu, kama watakuwa hawajasajili wakulima kufikia asilimia 85 kwa ajili ya kupata pembejeo za kilimo waandike barua za kuacha kazi.

Dendego alisema suala la kilimo katika Mkoa wa Singida ni jambo ambalo linatakiwa kupewa kipaumbele namba moja na hatakubali kuona wapo baadhi ya maofisa kilimo wanakwamisha jitihada za serikali katika kuinua sekta ya kilimo mkoani hapo.



Fundi akiendelea na ujenzi wa jengo la maabara ya masomo ya sayansi, kwenye Shule ya Sekondari Mtiro katika kijiji cha Busekera, Kata ya Bukumi, Musoma Vijijini mkoani Mara, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Milioni 50/- kumalizia ujenzi wa zahanati

**Na Mwandishi Wetu,** MKURANGA

SERIKALI imeipatia Zahanati ya Kijiji cha Mkokozi Sh. milioni 50 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi ili ifikapo mwaka 2025 ikabidhiwe kwa jamii hiyo.

Akizungumza katika hafla ya kuanza kwa ujenzi huo, Mganga Mfawidhi na Msimamizi wa mradi huo, Dk. Tatia Khan kutoka Zahanati ya Mwandege, alisema fedha hizo zimetolewa na serikali na wananchi wana wajibu wa kuhakikisha mradi huo unalindwa vizuri.

Alisema serikali itaunda kamati ya watu wanane ili kuhakikisha zahanati hiyo inakamilika kwa wakati.

"Jitahidini kuwa na moyo wa kujitolea ili tuweze kukamilisha zahanati hii. Tunahitaji pia nguvu kazi iongezeke," alisema.

Diwani wa Kata ya Mwandege, Nassoro Suleiman alisema mradi huo ni miongoni mwa mikubwa ya afya inayoendelea kutekelezwa chini ya ilani ya Chama cha Mapinduzi katika kata hiyo na maeneo mengine ndani ya Jimbo la Mkuranga.

Aidha, alisema katika kipindi cha miaka minne serikali imetoa fedha nyingi za ujenzi wa maboma ya zahanati, ujenzi wa shule za msingi na sekondari, miradi ya maji na uboreshaji wa miundombinu ya barabara katika kata hiyo.

"Tunamshukuru rais wetu na mbunge wetu Abdalah Ulega kwa kuhakikisha fedha zinapatikana za kutekeleza miradi ya kijamii kwa ajili ya maendeleo ya watu wa Mkuranga," alisema.

**Aidha, alisema zahanati hiyo itakuwa mkombozi mkubwa kwa wananchi wa Kijiji cha Mkokozi ambapo inatarajia kuhudumia wagonjwa kuanzia 500 hadi 600 kwa mwezi.**

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mkokozi, Ahmed Killo, alisema mradi huo umefikia hapo kwa juhudi za serikali na wananchi wa Mkokozi.

Alisema kutokana na mahitaji makubwa na matarajio ya wananchi wa Mkokozi mradi huo unahitaji kumalizika haraka angalau mwanzoni mwa mwaka kesho.

Killo alisema ili kuhakikisha mradi huo unakamilika haraka na kwa ufanisi, aliwataka wananchi kujifunga mkanda na kuwa walinzi namba moja wa mradi huo.

"Huu ni mradi wa maana sana. Wananchi wanahitaji kuheshimu nguvu za kwao na za serikali. Tutahakikisha tunatoa ushirikiano mkubwa kwa wazabuni," alisema.

Aidha, alisema zahanati hiyo itakuwa mkombozi mkubwa kwa wananchi wa Kijiji cha Mkokozi ambapo inatarajia kuhudumia wagonjwa kuanzia 500 hadi 600 kwa mwezi.

KABWELA — FADHILI MOHAMED



# Kampeni msaada kisheria ya Mama Samia yaanza tena

**Na Elizabeth Zaya**

KAMPENI ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia (MCLAC), imeanza tena kutolewa katika mikoa mingine minne mfululizo.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Huduma za Msaada wa Kisheria, Wizara ya Katiba na Sheria, Ester Msambazi, kampeni hiyo itafanyika kwa siku 10 mfululizo katika mikoa minne ya Morogoro, Iringa, Songwe na Mara.

Ester alisema kaulimbiu kwenye kampeni hiyo inasema 'msaada wa kisheria, usawa, amani na maendeleo' na imejikita zaidi katika kuimarisha upatikanaji wa haki kwa wananchi hususani wa kipato cha chini walioko pembezoni.

"Kampeni hii ambayo inaratibiwa na Wizara ya Katiba na Sheria, imehakikisha kuwa kila wilaya na halmashauri zote nchini zinapokea angalau wasaidizi wa kisheria watatu walio chini ya ofisi ya maendeleo ya jamii ambao wamepatiwa mafunzo maalum ili kutoa msaada wa kisheria wa hali ya juu," alisema Ester.

Alisema lengo kuu ni kuhakikisha huduma za kisheria, ambazo mara nyingi zinapatikana kwa gharama kubwa au kwa ugumu, zinafikishwa kwa urahisi na kwa uwazi kwa wananchi wote.

Alitaja malengo mengine ya kampeni hiyo kuwa ni pamoja na kuongeza ufahamu wa sheria, kuwafundisha wananchi kuhusu haki zao za kisheria na namna bora ya kuzitetea kupitia mfumo wa sheria.

Pia, kuwahamasisha wananchi kutatua migogoro kwa njia ya kisheria, kuwaelimisha kuhusu matumizi sahihi ya vyombo vya sheria kama mahakama na usuluhishi wa migogoro.

Kadhalika, inalenga kupunguza msongamano wa kesi mahakamani kupitia elimu ya sheria na upatanishi, na kwamba baadhi ya migogoro huitatua nje ya mahakama kupitia kampeni hiyo.

"Na pia inaweka nguvu katika kutoa msaada kwa makundi maalum ya wanawake, watoto na watu wenye ulemavu katika kuhakikisha wanapata msaada wa kisheria kwa changamoto zinazowakabili.

"Si hayo tu, bali inaleta manufaa kwa Watanzania kwa kuwahakikishia ufikikaji wa haki kwa wote, inachochea misingi ya haki sawa kwa wananchi wa vijijini na mijini, hususani wale wenye kipato cha chini na inaimarisha utawala wa sheria," alisema Ester.

Alisema, anaamini kupitia kampeni hiyo, wananchi watakuwa na uelewa zaidi wa mifumo ya sheria na umuhimu wa kuheshimu utaratibu wa kisheria, kukuza mshikamano wa kijamii kwa kutatua migogoro kupitia njia ya kisheria na kuimarisha amani katika jamii.

Aidha, kupitia kampeni hiyo, wanahamasisha ushirikishwaji wa jamii kikamilifu katika masuala ya kisheria, ikiwamo kutambua haki zao na wajibu wao, matumizi bora ya vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

"Kwa hiyo, vyombo vya habari vina nafasi muhimu katika kuhakikisha kampeni hii inafanikiwa kwa kufikisha ujumbe kwa walengwa na kuhamasisha ushiriki wa jamii," alisema Ester.



Sehemu ya wahitimu, wakiwa kwenye mahafali ya 18 ya Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## Jaji Mwaimu: Malalamiko Uchaguzi wa Serikali za Mitaa yasipuuzwe

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MWENYEKITI wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Jaji mstaafu Mathew Mwaimu, amesema malalamiko kuhusu uendeshaji wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa yasipuuzwe bali yatumike kama tafakari ya kuondoa kero zilizojitokeza zisijirudie kwenye Uchaguzi Mkuu mwaka huu.

Jaji Mwaimu alitoa kauli hiyo jana wakati wa maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu yaliyofanyika jijini hapa, akisema amesikia kupitia vyombo vya habari malalamiko kuhusu uchaguzi huo na rai yake ni kwamba yasipuuzwe.

"Ningependa kusema jambo moja, nimeona kupitia vyombo vya habari kuhusu malalamiko ya wagombea kuenguliwa na changamoto nyinginezo zilizojitokeza wakati wa upigaji kura na wakati wa kutangaza matokeo," alisema.

"Sisi kama watendaji ambapo baadhi yetu tulisimamia uchaguzi huo wa serikali za mitaa, tusipuuze malalamiko hayo na tunatakiwa kuyatafakari na kuyafanyia kazi ili changamoto hizo zilizojitokeza kwenye uchaguzi huo zisijitokeze tena katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025," alisema.

Jaji Mwaimu pia aliwataka watumishi wa umma kufanya kazi kwa uadilifu na kuacha kufanya kazi kwa mazoea na watoe huduma bora kwa wananchi.

Awali Katibu wa Tume hiyo, Mathew Kirama alisema siku hiyo ya haki za binadamu huadhimishwa kila mwaka inapotimu Desemba 9 ikiwa ni utekelezaji Mkataba wa Kimataifa wa Kupambana na Rushwa wa Mwaka 2003.

Kirama alisema kutokana na nchi kuadhimisha uhuru wa Tanzania Bara tarehe hiyo, serikali kuanzia mwaka 2016 iliamua kuadhimisha siku hiyo pamoja na Siku ya Kimataifa ya Haki za Binadamu kila Desemba 10 na tamko la Baraza la Umoja wa Mataifa la Mwaka 1948 kuhusu haki za binadamu.

Alisema maadhimisho hayo yamekuwa yakiratibiwa kwa pamoja na taasisi zinazosimamia mapambano ya dhidi ya rushwa, haki za binadamu na utawala bora nchini.

Alitaja taasisi hizo kuwa ni Ofisi ya Rais - Ikulu, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Wizara ya Katiba na Sheria, Sekretarieti ya Maadili, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Tume ya Utumishi wa Umma.

Taasisi zingine ni Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA), Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT), Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali.

Naibu Mkurungenzi wa TAKUKURU, Neema Mwakalyelye aliwahimiza kuzingatia maadili ya utumishi wa umma ili kuleta ustawi wa umma.

## Serikali kutoa elimu kulingana maendeleo kiteknolojia

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

SERIKALI imesema inajitahidi kutoa elimu kulingana na maendeleo ya teknolojia ili kuleta matokeo chanya ikiwamo kutumia Akili Mnemba ili kwenda na kasi ya mabadiliko yanayofanyika duniani ili Tanzania isiweze kuachwa nyuma kimaendeleo.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Daniel Mushi, alisema hayo wakati akifungua Kongamano la Kimataifa la Taaluma ya Maendeleo linalohusisha vyuo vikuu vya ndani na nje ya nchi linalofanyika kwa siku mbili mkoani hapa.

Kongamano hilo limeandaliwa na Chuo Kikuu cha Mzumbe lenye kaulimbiu; 'Mtazamo wa Maendeleo kwa kizazi cha sasa na kijacho".

Naibu Katibu alisema teknolojia ina fursa kubwa ya kuharakisha maendeleo kama ikutumika ipasavyo ndio maana kama serikali inajitahidi kuhakikisha elimu inayotolewa inaendena na mabadiliko ya teknolojia ya duniani.

"Tunajitahidi sana kuhakikisha elimu tunayotoa inaendana na mabadiliko ya teknolojia yanayotokea duniani ili tusiachwe nyuma, kwa kuwa teknolojia ikutumika vizuri inaweza kunufaisha jamii, lakini ikitumika vibaya inaweza kuiyumbisha jamii," alisema.

Alisema kulingana na mabadiliko ya teknolojia duniani Tanzania ikiwa na wataalamu wenye ujuzi watasaidia kuamua teknolojia zipi zitumike kuleta faida na kuepuka madhara yanayotokana nazo.

Alisema maendeleo ya nchi hayawezi kupatikana bila ushirikishwaji wa sekta mbalimbali ikiwamo serikali kushirikiana na sekta binafsi pamoja na wadau wa maendeleo na kila mmoja kwenye utatu anapaswa kuwa na mtazamo sahihi.

Naye Makamo Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe (MU), Profesa William Mwegoha, alisema kongamano hilo linaangalia muktadha wa taaluma za maendeleo katika ulimwengu unaoendelea kubadilika katika kiazazi cha sasa na kijacho.

Alisema wanakutana wakiwa na lengo la kuangalia taaluma za kimaendeleo katika ulimwengu wa mabadiliko ikiwamo teknolojia, uchumi na changamoto mbalimbali, mabadiliko ya tabianchi na kuangalia taaluma za maendeleo zifanyiwe mapitio ili ziendelee kuwa na thamani.

Naye Mkurugenzi wa Taasisi ya Taaluma za Maendeleo, Profesa Elizabeth Lulu Genda, alisema hilo ni kongamano la tatu la kimataifa limekuwa na mijadala wa maendeleo kwasababu yanabadilika kwa kadri miaka inavyoenda.

Alisema lengo ni kumlenga Mtanzania kujitambua na kujua kuwa maendeleo yanahusu yeye binafsi na kutunza zile rasilimali zilizopo hapa nchini kwa manufaa ya kizazi kijacho.

Kongamano hilo la Kimataifa la tatu ni ushirikiano wa vyuo vikuu vitano, ikiwamo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo Kikuu cha Afya (MUHAS), Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).



## Barabara Moshi- Arusha kufumuliwa

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

SERIKALI inatarajia kutumia zaidi ya Sh. bilioni 5.8 kwa ujenzi wa eneo hatarishi la barabara kuu ya Moshi- Arusha wakati wa mvua.

Ni baada ya serikali kuingia mkataba na Kampuni ya ujenzi ya KINGS BUILDERS LTD ya Dar es Salaam ya kufumua barabara hiyo katika eneo hilo la kwa 'Wasomali' lililoko wilayani hapa Mkoa wa Kilimanjaro.

Mradi huo wa dharura wa kuboresha/kurekebisha miundombinu iliyoathiriwa na mvua za El-Nino, pia utahusisha ujenzi wa madaraja saba na kunyanyua tuta la barabara kimo cha mita 1.5 katika maeneo yenye urefu wa mita 500 na mita 1,725.

Akizungumzia ujenzi huo wakati wa makabidhiano ya mradi na mkandarasi huyo, Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) Mkoa wa Kilimanjaro, Benitho Mdzove, alisema mkoa huo ni kati ya mikoa iliyoathiriwa na mvua za El-Nino zilizonyesha nchini kuanzia mwishoni mwa mwaka jana hadi mwanzoni mwa mwaka huu.

Mdzove, alisema serikali imepata fedha hizo kutoka Benki ya Dunia (WB) kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya madaraja katika maeneo yaliyoathiriwa na mvua hizo mkoani humo.

Alisema mvua hizo zilileta athari mbalimbali katika miundombinu ya barabara kwa kuharibu vibaya mtandao wa barabara ya Mkombozi (KLM)-Tanga (Border), Himo Njiapanda - KIA Njiapanda.

Diwani wa Kata ya KIA, Tehera Mollel, alisema eneo hilo linalojengwa madaraja mapya saba, limekuwa kero kipindi cha mvua hizo za masika.

Mollel, alisema pamoja na eneo hilo kukumbwa na mafuriko, maji yamekuwa yakiharibu mashamba ya wakulima na kusomba mazao na baadhi ya magari barabarani.

Mkuu wa Mkoa huo, Nurdini Babu, alimtaka mkandarasi huyo kuanza ujenzi huo mara moja na kuonya visingizio kutumika kama kinga ya kuchelewa kukamilika kwa mujibu wa mkataba Septemba 25, mwakani.

# Mgombea wa CHADEMA adai utashi umemponza

**Na Oscar Assenga,** TANGA

KATIBU mstaafu wa Baraza la Vijana wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Mkoa wa Tanga, Hemed Said, amedai 'utashi' wake wa kujitokeza kupongeza uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji umemweka matatani.

Akizungumza na Nipashe, Hemed, ambaye alichukua fomu ya kugombea uenyekiti wa mtaa kisha kuwekewa pingamizi na kuondolewa kwa kukosa sifa, alidai tuhuma ameshiriki kuihujumu CHADEMA katika uchaguzi huo, hazina mashiko.

"Nina wasiwasi kwa sababu nimekuwa nikipata vitisho kutoka kwa baadhi ya wezangu, wakiwamo viongozi na wanachama wa chama changu kwamba nahusika kuihujumu CHADEMA.

...Siwezi kuhusika kwa namna yeyote kukihujumu chama, hivyo naomba nijivue. Kwa sababu nipo ndani ya chama kwa zaidi ya miaka 15 na ninafahamu taratibu miongozo na kanuni zinazohusu uendeshaji wa chama," alidai.

Inadaiwa kuwa Hemed alikihujumu CHADEMA baada ya kushiriki kikao cha viongozi wa siasa Wilaya ya Tanga na kupongeza mchakato wa uchaguzi huo wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji uliofanyika Novemba 27, mwaka huu.

**Akizungumza na Nipashe, Hemed, ambaye alichukua fomu ya kugombea uenyekiti wa mtaa kisha kuwekewa pingamizi na kuondolewa kwa kukosa sifa, alidai tuhuma ameshiriki kuihujumu CHADEMA katika uchaguzi huo, hazina mashiko.**

Alidai alipokwenda kwenye kikao hicho kama mmoja wa wagombea, maoni aliyoyatoa ni kama mgombea aliyeenguliwa kwenye uchaguzi huo.

"Sasa hapo mimi ninahusikaje na tuhuma za kuuza, kuharibu mipango au kukwamisha shughuli zozote za mafanikio ya chama changu?" Alihoji.

Alidai hakuna utaratibu wa kichama uliofuatwa, ikiwamo kumwita kwa njia ya barua kumhoji kuhusiana na tuhuma hizo.

CHADEMA Wilaya ya Tanga katika uchaguzi huo ilisimamisha wagombea 50 kati ya hao wanane walijitoa wakati mchakato wa uchaguzi huo.

"Ndani ya chama chetu katika Halmashauri ya Jiji la Tanga, tuna mitaa 181 tulikuwa na wagombea 50. Tulikuwa na mawakala 182, Je, kwa nini hawa wanane na mimi (Hemed). Ni nani amerubuniwa? kama walijitoa chama kimewachukulia hatua gani mpaka mimi nionekane kama ninahusika moja kwa moja?," aliendelea kuhoji.



Mbunge wa Afrika Mashariki, James Ole Millya (kushoto) na Ofisa Madini Mkazi Mirerani, Nchagwa Chacha Marwa, wakizungumza na wawekezaji raia wa China walipotembelea migodi ya madini ya Tanzanite katika mji mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wamasai rukhsa kuoa wa kabila lingine

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAKATI leo ni kilele cha siku 16 za wanaharakati kupinga ukatili wa kijinsia duniani, wazee wa mila wa jamii ya kifugaji ya Kimasai (malegwanani) ukanda wa chini wa Moshi mkoani Kilimanjaro wamelegeza masharti ya ndoa kwa vijana wao kwa wanaowapenda.

Uamuzi huo unatengua sheria yao ya kimila ya kuwachagulia vijana wa kiume mke wa kuoa na wa kike kuolewa na mume anayetoa posa tangu akiwa mtoto hata kama hajampendea.

Kiongozi wa mila wa jamii hiyo, Legwanani, Isaack Daudi akizungumza jana katika Kijiji cha Mserekia, Kata ya Mabogini wakati wa mdahalo wa elimu ya kupinga ukatili katika jamii, alisema kwa sasa suala la kuolewa au kuoa kwa maamuzi yao, hawana tatizo nalo, hivyo ni sahihi kwa kijana au msichana wa Kimasai kufanya hivyo.

Mdahalo huo unaendeshwa kupitia Mradi wa Sauti ya Haki unatekelezwa na Shirika la KWIECO kwa ufadhiliwa na Women Fund Tanzania Trust (WFT).


Michael Maningo, ambaye kiongozi wa mila wa rika la vijana, alisema kwa sasa ni furaha kwa vijana wa kiume kuoa mke anayempenda kutoka kabila lao au jingine na msichana kuolewa na mwanamume ampendaye.

Ismail Abdilah akizungumza katika mdahalo huo alisema kuwa: "Ndani ya miaka mitano, mabadiliko makubwa yametokea katika kata yetu ya Mabogini, vitongoji 45, vijiji vyake vinane ikiwamo Mserekia," alisema na kuongeza kuwa: "Zamani wenzetu wa jamii ya Kimasai, wanawake walikuwa hawaruhusiwi kufanya kazi za kujitafutia kipato, lakini kwa sasa anaruhusiwa na ana sauti na anasikilizwa kwenye familia."

Legwanani Abel Lenana, alipongeza KWIECO na wadau wengine kwa elimu wanayoitoa ya haki za binadamu na usawa wa kijinsia ndani ya jamii kuleta mabadiliko hasa kwa jamii ya wafugaji ikiwa ni pamoja na kuachana na mila na desturi zisizofaa za kukeketa watoto wa kike na kuwaozesha katika umri mdogo.

Mratibu wa Mradi wa Sauti ya Haki, Veronica Ollomi, alisema elimu ya usawa wa kijinsia na haki za binadamu kwa Wamasai waliyoipata, inatoa haki kwa rika hilo kufanya maamuzi juu ya maisha yao.

Kwa mujibu wa mratibu huyo, uamuzi huo utasaidia kuwawezesha wanawake kushiriki kwenye shughuli mbalimbali za kujiongezea kipato, kushiriki ngazi za maamuzi na kuboresha maisha ya familia.





# Zaidi ya 2,000 wachangamkia matibabu madaktari bingwa

**Na Vitus Audax**

WAGONJWA zaidi ya 2,000 wamepatiwa matibabu na madaktari bingwa 42 nchini katika Hospitali ya Rufani ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Kwangwa iliyopo mkoani Mara.

Kati ya hao 2,244, wagonjwa 74 walifanyiwa upasuaji, 46 kupatiwa rufaa ya kupata matibabu zaidi katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando.

Akihitimisha kambi hiyo siku tano juzi, Katibu Tawala wa Mkoa wa Mara, Gerald Musabila alisema madaktari hao wakiwamo wa mkoa huo, wametoa matibabu kwa wagonjwa hao baada ya kujitokeza tangu ilipoanza.

"Wananchi wa Mkoa wa Mara wanawashukuru sana na wangependa mwendelee kutoa huduma hapa, lakini wanafahamu huko mlipotoka pia wanawahitaji watu wengine kupata huduma," alisema Kusaya.

Katibu Tawala Msaidizi Afya, Lishe na Ustawi wa Jamii, Dk. Zabron Masatu, alisema katika kambi hiyo, wamekusanya Sh. milioni 186, fedha taslimu na bima za afya.

"Hospitali imetumia Sh. milioni 30 kwa ajili ya kulipa stahiki za watumishi wa Hospitali ya Rufani ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere walioshiriki kwenye kambi hii na maandalizi ya kambi hiyo," alisema Dk. Masatu.

**Kati ya hao 2,244, wagonjwa 74 walifanyiwa upasuaji, 46 kupatiwa rufaa ya kupata matibabu zaidi katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando.**

Alizishukuru hospitali za mikoa ya kanda ya ziwa na za rufani kanda za Chato na Bugando kwa kuwaruhusu na kuwawezesha madaktari hao kushiriki katika kambi hiyo.

Aliwashukuru viongozi wa mkoa huo, wa Mara, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Wizara ya Afya kwa kuandaa na kuratibu kambi hiyo.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Dk. Osmund Dyegura alisema kambi hiyo ilianza mwaka 2022 katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Simiyu.

Dk. Dyegura alisema mbali na Mkoa wa Simiyu, kambi hiyo imewahi kufanyika katika Mkoa wa Kagera na sasa Mara kwa wananchi kwa kuwapatia huduma.

Alisema lengo la kambi hiyo ni kusogeza huduma za kibingwa jirani na wananchi, kuwajengea uwezo wataalamu wa afya, kuibua wagonjwa ambao watapelekwa kupata matibabu zaidi katika hospitali za rufani za kanda.




Wenyeviti wa vijiji vilivyoko jirani na mgodi wa dhahabu wa North Mara, wakionesha mifano ya hundi za malipo ya gawio la mrabaha la Sh. bilioni 2.1, lililotolewa na mgodi huo juzi, baada ya kukabidhiwa na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima (wa tatu kushoto waliokaa). Katikati ni Meneja Mkuu wa Mgodi huo, Apolinary Lyambiko. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mhifadhi TFS aiumbua Kahama upandaji miti

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MHIFADHI Mwandamizi wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) wilayani hapa Mkoa wa Shinyanga, Esther Msokwa ameiumbua Kahama kuwa haina utaratibu wa upandaji miti licha ya kuwa wakataji wazuri wa miti.

Msokwa alitoa kauli hiyo juzi wakati wa kampeni ya upandaji miti katika Shule ya Sekondari Anderson Msumba ikiwa ni sehemu ya Maadhimisho ya Miaka 63 ya Uhuru na kuwataka walimu na wanafunzi kuwa mfano kuhimiza upandaji miti na kuitunza katika maeneo yao.

Alisema hali hiyo inahatarisha mstakhabari wa mazingira wilayani hapa na kuwataka wananchi na taasisi kutumia nishati mbadala ya kupikia ya gesi safi ili kudhibiti ukataji miti ovyo.

Msokwa alisema katika shule hiyo wamepanda miti 200 eneo la wazi na kuwataka walimu na wanafunzi kuitunza na kuhamasisha wanafunzi kuwa na desturi ya kupanda miti maeneo ya nyumbani kwao.

"Kukata miti sio shida bali shida inakuja unaukata kwa utaratibu gani," alisema na kuongeza kuwa:

"Watu kipindi cha masika hawapandi miti ambao ndio kipindi kizuri cha upandaji na kustawi."

Ofisa Mazingira Manispaa ya Kahama, Edberth Momoyi, aliwataka walimu wa shule hiyo kusimamia utunzaji mazingira na sheria ndogo ndogo dhidi ya watu wanaoingiza mifugo kwenye maeneo yaliyopandwa miti.

Mkuu wa Shule hiyo, James Kiboko, alisema wameanzisha klabu ya mazingira shuleni hapo kwa ajili ya kutunza mazingira.

Kiboko, alisema katika klabu hiyo, kila mwanafunzi ana mti ambao anautunza kuanzia akiwa kidato cha kwanza hadi cha nne, anapomaliza na kukabidhi ukiwa umestawi.

Baadhi ya wanafunzi wa shule hiyo walioshiriki upandaji miti huo, akiwamo Jackline Samwel, waliahidi kuwa walinzi na mabalozi katika utunzaji wa mazingira na kuwashtaki waharibifu.

# DC Mtatiro ahadharisha vijana Ukimwi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Wilaya ya Shinyanga mkoani hapa, Julius Mtatiro amewahadharisha vijana kujikinga na maambukizi ya Ukimwi kwa kupima afya kabla ya kuingia kwenye mahusiano ili kuepuka maambukizi ya virusi hivyo.

Mtatiro alitoa hadhari hiyo juzi baada ya kupima virusi hivyo Maadhimisho ya Miaka 63 ya Uhuru kimkoa na kuwataka vijana kuacha kuishi kwa mazoea.

"Msiogope kupima VVU (Virusi Vya Ukimwi). Mimi nimejitokeza na nimepima hapa hadharani kila mtu ananiona, ila majibu ni siri yangu na mpimaji," alisema na kusisitiza kuwa:

"Na wasihi vijana jengeni tabia ya kupima Virusi Vya Ukimwi na wapenzi wenu kabla ya kuingia kwenye mahusiano ili mjue hali zenu kiafya na kuendelea kuwa waaminifu kwenye mapenzi yenu."

Mtatiro, alisema mtu akijua afya yake, itasaidi kujilinda zaidi na kuepukana na ugonjwa kuambukizwa Ukimwi baada ya kupewa ushauri nasaha namna ya kuchukua tahadhari na kuendelea kuwa salama.

Aliwakumbusha wananchi katika msimu wa mvua kuchukua tahadhari kwa kudhibiti mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu kwa kunawa mikono kwa sabuni wakati wa kula, kuchemsha maji na kuchimba vyoo vya kisasa na kuvitumia.

Kuhusu maendeleo tangu kupatikana kwa Uhuru, Mtatiro, alisema mwaka 1961 Mkoa wa Shinyanga haukuwa na viwanda, lakini hadi sasa una vikubwa 40, kati 192 na vidogo 1,225.

Alisema mkoa huo wakati huo na umeme, kwa sasa vijiji 485 vina huduma hiyo, shule za awali na msingi 635 na 15 za wanafunzi wenye ulemavu zimejengwa.

Akizungumzia kuhusu sekta ya maji, Mtatiro, alisema kulikuwa na visima 16, lakini sasa wananchi wa mjini wanapata maji asilimia 73 na vijijini 68.

Baadhi ya wazee akiwamo Spora Pangani, walisema kabla ya nchi kupata uhuru, watu walikuwa wakiishi kama wanyama chini ya wakoloni, tofauti na sasa maisha yameboreshwa kwa kupata huduma zote muhimu.



Ukurasa 12

**Afrika Mashariki ndani ya usukani wa Dk.Ruto**



Ukurasa 13

Ndizo hasi, chanya kuendeleza demokrasia miaka 63 ya uhuru



Ukurasa 14

**Baada ya kutimuliwa Syria, Assad ajisalimisha kwa Putin**


# siasa

JUMATANO DESEMBA 11, 2024

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU


# Miaka 63 ya uhuru na matamanio ya kuinusuru SGR na kukatika umeme

**Na Gaudensia Mngumi**

MIAKA 63 ya Uhuru wa Tanganyika imetimia na katika sekta ya usafirishaji serikali imefanya mengi ikiwamo kujenga reli ya kisasa na pana maarufu kama SGR. Ni jambo la kihistoria.

Mafanikio ya SGR yatapatikana iwapo itaweza kusafirisha shehena kubwa na nyingi ya Congo DRC, Uganda, Zambia, Malawi, Zimbabwe na Tanzania yenyewe.

Lakini ni mradi unaohitaji umeme wa uhakika ili kusonga mbele bila kutetereka kwani nishati hiyo ni kila kitu.

Ili kupata mafanikio na mavuno ya matunda ya uhuru kwenye reli hiyo, shirika la TANESCO lijenge gridi maalumu itakayotumika kwenye usafirishaji wa reli ili kufanikisha mikakati na maono ya kuwa miundombinu bora katika ukanda huu.

Anasema Dk. Peter Kafumu, mtaalamu wa nishati na madini, anapozungumzia mambo ya kujivunia ndani ya miaka 63 ya uhuru kwenye sekta za usafirishaji akigusia SGR kwenye kusafirisha abiria na shehena.

“Tunahitaji kuwa na gridi maalum kutoka vyanzo vingine kama joto ardhi, upepo, jua na gesi kwa ajili ya kulisha usafirishaji huo,” anasema.

Gridi ya umeme ni mtandao unaohusisha kuzalisha au kufua kutoka vyanzo mbalimbali, kukusanya pamoja na kusambaza kwa wateja.

Anafafanua kuwa ni kwasababu utahitajika umeme wa kutosha kupeleka bidhaa ndani na nje ya nchi zikifika Mpanda, Mwanza, Burundi hadi Uganda.

“Hapo ndipo kinapohitajika chanzo kingine mahsusi na gridi maalumu.” Anashauri Dk. Kafumu aliyewahi kuwa Kamishna wa Madini.

Anasema kutegemea gridi ya taifa kama ilivyo sasa kunaweza kuleta changamoto kwenye usafirishaji wa reli hiyo na kwamba ikiwezekana serikali ikope fedha kujenga chanzo na kutenga gridi hiyo isiyotegemea ile ya taifa.



Ubora na ufanisi wa treni hii ni kuwapo umeme wa uhakika kuiendesha kusafirisha abiria na shehena. **PICHA: TRC**

Anaeleza kuwa Ulaya mfano Ufaransa na Ubelgiji umeme unaotumika kuendesha treni hizo na za mijini zina gridi maalumu iliyojengwa kulisha sekta hiyo pekee.

Anataja Ubelgiji kuwa usafirishaji mijini unategemea ‘trams’ au mabasi yanayopita juu ya reli yakitumia umeme muda wote na kwamba nishati yake haiingiliani na matumizi mengine akipendekeza Tanzania kufanya kama taifa hilo.

“Tuwe na chanzo chenye megawati kuanzia 200 kuendesha SGR yetu isitegemee gridi ya taifa.”

Dk. Kafumu anakumbusha kuwa Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere ambalo ni tegemeo la SGR linazalisha umeme wa maji ambao unaweza kuathirika na changamoto za kimazingira.

“Yapo mabadiliko ya tabianchi na ukame wa muda mrefu vinaweza kuwa kitisho kwenye umeme wa maji. Nashauri kufikiria njia bora ya kuwa na gridi mahususi ya SGR,” anasema.

Anasisitiza kuwa pamoja na kutumia reli hiyo ya umeme ni vyema pia ile ya zamani ya MGR inayokwenda Mwanza, Kigoma, Kilimanjaro na Tanga itanuliwe na kuongezewa ukubwa ili kusafirisha bidhaa na abiria.

Anakumbusha kuwa marekebisho ni lazima kwa miundombinu hiyo, akisema usafirishaji wa reli ni muhimu duniani kote.

Akizungumzia maendeleo ya nishati na jubilii ya uhuru, Dk. Kamugisha Byabato, anasema kinachohitajika si gridi mpya ya SGR bali ni TANESCO kubadilika na kuwajibika.

Anashauri iwajibike kwenye hasara zinazotokana na kukatika ovyo kwa umeme hata kwa nusu dakika na kwamba kitakuwa kufidia hasara ili iwe makini zaidi.

Anasema miaka 63 ya uhuru suala la nishati ya uhakika siyo la kupuuzwa ni lazima iwepo kwa ajili ya maendeleo ya kila kitu na kufanikisha mikakati inayopangwa na wateja wadogo hadi wakubwa.

Anasema kuwapo kwa SGR kunalenga ulazima wa kuwa na umeme wa kutosha kuendesha treni hiyo tena mifumo ya kuiwezesha kutembea na kufanya kazi kwa uhakika kwa ajili ya kufanikisha kubeba shehena na abiria wa ndani na nje ya nchi na kuzuia isikwame au kusimama ghafla.

“Niseme kuboresha umeme ni lazima na kukatikakatika umeme ghafla kuishe kusiweko tena na shida hiyo tunapoelekea miaka mingine ijayo.” Anasema.

Dk. Byabato mhadhiri wa vyuo vikuu kikiwamo cha Dar es Salaam, Ardhi na sasa SAUT anasema SGR haihitaji gridi yake pekee bali TANESCO kuwa na mbinu za kuuzuia umeme uliopo usikatike ovyo, kuwa na uangalizi wa mitambo ya kuufua na kuutunza usiachwe kuvuja bila kujali.

Dk.Byabato anaamini kuwa hilo linalowezekana kwa kutumia teknolojia na kuhakikisha kuwa athari kwa reli ya SGR zinakomeshwa.

Anasisitiza kutumia vituo vya umeme vilivyopo na kujenga vingine ili kuweka akiba ya umeme utakaoendesha SGR na pia kutumia teknolojia na miundombinu bora inayolinda treni ili umeme ukikatika usiumize vyombo vya usafiri kama reli hiyo.

“Teknolojia zipo za kuwa na mifumo bora na vituo vya kutunza umeme wa akiba ili endapo mwingine utakatika utumike kutoka stesheni nyingine zinazotunza wa akiba ili kuendesha usafiri wetu.” Anaongeza.

### KUBORESHA UMEME

Akirejea maendeleo ya upatikanaji nishati ndani ya miaka 63 ya uhuru Dk. Byabato injinia wa teknolojia na nishati nyadidifu anasema kwenye kipindi hicho kuna vitu vilitakiwa kufanyika mara baada ya uhuru mojawapo ni kuvipatia vijiji umeme.

“Umeme kwa kila kijiji ulitakiwa kufanyika mapema zaidi si baada ya miaka 50 ya uhuru. Ni mambo ya kitaifa yaliyohitaji kutekelezwa mapema ili kufanikisha elimu, tiba, uzalishaji hasa viwanda vidogo kwa vikubwa, kutoa huduma za mawasiliano zikiwamo simu. Kwa ujumla kuharakisha maendeleo.”

Anatoa angalizo kuwa ili umeme vijijini uwe endelevu ni lazima taifa lizalishe mafundi umeme kwa kila kijiji ili kudhibiti kukatika, kuanguka nguzo na kulipuka transfoma.


**INAENDELEA UK. 12**

# Afrika Mashariki ndani ya usukani wa Dk.Ruto

**Na Mwandishi Wetu**


RAIS wa Kenya, William Ruto, hivi karibuni amekabidhiwa kiti cha kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), akichukua nafasi hiyo kutoka kwa mwenzake, Rais wa Sudan Kusini, Salva Kiir, baada ya muhula wa mwaka mmoja kukamilika.

Ruto ndiye msimamizi wa jumuiya hiyo, yenye wanachama wanane, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Kenya, Rwanda, Somalia, Sudan Kusini, Tanzania na Uganda

Kwa nafasi hiyo, Ruto ataiongoza jumuiya kwa kipindi cha mwaka mmoja, wa mujibu wa kanuni za EAC kuhusu uongozi wa uenyekiti.

Hivi karibuni jijini Arusha, kwenye mkutano wa 24 wa Marais wa Mataifa wanachama wa EAC, Rais Ruto, kwanza alimpongeza mtangulizi wake akisema ni 'uongozi wenye kuigwa' kwa kuwa ulisheheni maono.

"Chini ya uongozi wake, jumuiya ya EAC imepiga hatua kubwa katika kuendeleza misingi ya utangamano," nasifu Rais Ruto.


Rais William Ruto ndiye Mwenyekiti wa EAC. **PICHA: MTANDAO**

### AJENDA ZA KUSIMAMIA

Rais Ruto anachukua uenyekiti wa jumuiya hiyo kwa kuzingatia ajenda ya wanachama wote wanane kwa kubuni utangamano wa kisiasa.

"Ndoto ya utangamano wa kisiasa katika EAC ni safari ya kipekee ya kuunganisha eneo hili," Rais Ruto, anasema huku akitaja kuwa kuna changamoto ambazo lazima zikabiliwe, ili kufikia lengo hilo.

Rais Ruto anasema kuna manufaa makubwa katika umoja wa kisiasa baina ya mataifa hayo, wanachama wa EAC, kuliko changamoto.

"Sharti kujizatiti kufaidi kutokana manufaa yanayoletwa na hatua hii ili kujenga EAC thabiti ambayo itawezesha kubuniwa kwa soko la pamoja barani Afrika," anaeleza.

Rais Ruto anaahidi kuwa wakati wa hatamu yake kama mwanachama wa EAC, ataipa kipaumbele ajenda ya kuboresha maisha ya watu wa kwenye ukanda huo wenye takribani watu milioni 332.

Takwimu za tovuti kadhaa mtandaoni zinabainisha kuwa idadi ya watu wake imeendekea kukua kwa kasi kutoka milioni 127.4 mwaka 1990 hadi 332 mwaka jana.

Hata hivyo, inakadiriwa kuwa idadi itakua na kufikia watu milioni 560 ifikapo mwaka 2043.

### UZALISHAJI BIDHAA

Rais Ruto anasema kuwa nguzo kuu kwa EAC ni muhimu kuupiga jeki uchumi za mataifa wanachama, kwa kuongeza nafasi za ajira na kufikia malengo ya maendeleo katika ukanda huo.

"Tutalenga kuimarisha ubora wa bidhaa zinazozalishwa, kuendeleza mpango wa uongezaji wa thamani mazao ya shambani, tutaendeleza biashara miongoni mwa mataifa ya ukanda huu na kuimarisha uwekezaji," anaahidi.

Mwenyekiti huyo mpya wa EAC anashauri kuwa mataifa wanachama yanapaswa kuondoa vikwazo vya kibiashara baina yao.

"Sharti mataifa ya EAC yaondoe vikwazo kama vile ushuru wa juu kwa bidhaa zinazoingizwa katika nchi wanachama, tuimarishe miundo msingi na tulenge kuoanisha sheria mbalimbali za kibiashara."

Anasema atahakikisha anaongeza ushindani wa kibiashara, kukuza uzalishaji na uongezaji thamani wa bidhaa za ndani ya jumuiya hiyo.

Aidha, anaeleza vipaumbele kwamba ni kuongeza imani miongoni mwa nchi wanachama na kuimarisha uwekezaji kwa faida ya uchumi EAC.

"Hivi ndivyo vipaumbele vyangu vya muhimu kwa ajili ya kuleta mageuzi ya uchumi wa EAC, kutengeneza ajira na kuhakikisha kuna maendeleo endelevu kwa nchini zote, amani, usalama na utulivu," anasema.

Anasisitiza pia kusimamia suala la uwajibikaji wa kisiasa na utawala bora kwa kuwa ndiyo njia bora ya kuhakikisha uwapo wa utulivu endelevu katika jumuiya hiyo.

Rais Ruto, anaongeza kuwa ili kufikia hayo yote ni lazima EAC kuendelea kuimarisha mifumo ya kikanda ambayo inalinda mamlaka yao na usalama wa pamoja, huku akihimiza utawala jumuishi unaoakisi matarajio ya wananchi wa Afrika Mashariki.

"EAC ni jumuiya yenye soko kubwa kutokana na kuwa na idadi kubwa ya watu zaidi ya milioni 300 linalotoa fursa ya kujenga uchumi na kuimarisha biashara kwa manufaa ya watu wa EAC," amesema.

Kadhalika, hakuiweka kando lugha ya Kiswahili kujumishwa na za kimataifa akitaja Kiingereza na Kifaransa, kuwa zitaendelea kutumika EAC, huku akisisitiza Kiswahili kitabeba utamaduni wa watu wa jumuiya.

### ILIKOTOKA EAC

Jumuiya ya Afrika Mashariki ni ya kikanda ya kiutawala inayoanzishwa ili kukuza ushirikiano wa kiuchumi na utangamano katika Afrika Mashariki.

Chimbuko la EAC lilianzia mwanzoni mwa miaka ya 1900, wakati Kenya, Uganda na Tanganyika (sasa Tanzania) zilipoanzisha uhusiano wa vyama vya ushirika, uliojumuisha Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki mwaka 1905 na Shirika la Reli na Bandari la Afrika Mashariki 1948.

EAC ya kwanza ilianzishwa mwaka 1967 na marais wa Kenya, Tanzania na Uganda, hata hivyo, ilivunjwa mwaka 1977 kutokana na kutofautiana kwa sera za kisiasa na kiuchumi miongoni mwa nchi wanachama.

Ilirejea upya mwaka 1999, Kenya, Uganda na Tanzania zikianza tena mazungumzo na kusaini mkataba wa kuanzishwa kwake. Mkataba huo ulianza kufanyakazi Julai 2000 na kuanzisha tena EAC. Kuhusu wanachama wapya, Rwanda na Burundi zilijiunga na EAC mwaka 2007, Sudan Kusini 2016 wakati Somalia ilikaribishwa 2024, chombo hicho kikiwa na makao makuu Arusha, Tanzania.

Miongoni mwa mafanikio ya EAC ni pamoja na kuwako Umoja wa Forodha ulianza mwaka 2005, ambao hurahisisha usafirishaji wa bidhaa ndani ya kanda, lipo Soko la Pamoja (2010), ambalo hurahisisha kuhamisha watu, wafanyakazi, huduma.

Pia kuwapo mitaji ndani ya kanda Umoja wa Fedha 2013, ambao unalenga kuanzisha sarafu moja, jengo la Taasisi ya Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi, Sauti ya pamoja katika mikutano ya bara na kimataifa. **MTANDAO**

## Miaka 63 ya uhuru na matamanio ya kuinusuru SGR na kukatika umeme

**INATOKA UK. 11**

"Tulitakiwa pamoja na mradi wa Umeme Vijijini REA tuwe na mafundi umeme vijijini, kwani inawezekana ukakatika kwa zaidi ya siku 10 bila kasoro kurekebishwa kwa sababu hakuna mafundi."

Anashauri kuwe na programu ya kufundisha mafundi umeme vijijini na kwamba utekelezaji wa dira ya maendeleo ya taifa 2050 ifanikishe upatikanaji wa mafundi wa ngazi mbalimbali watakaowahudumia wananchi.

### NISHATI KITAIFA

Dk. Byabato anasema kitaifa bado umeme haujakaa sawa kwenye upatikanaji wa nishati hiyo kwa uhakika na kwamba kuna ulazima wa kuwasikiliza wataalamu ili kumaliza changamoto za nishati na umeme.

"Nashauri wanasiasa wawasikilize wataalamu tusiamue mambo ya nishati bila utaalamu, kufanya mambo kisiasa zaidi kunapunguza ufanisi na mafanikio."

Anaonya kuwa wakati mwingine wataalamu wanaposhauri mambo wanaonekana kama wanabishana na viongozi na wanapotofautiana mwanasiasa anachukua hatua ambazo zinaathiri wataalamu.

Akizungumzia vyanzo mbadala vya nishati anashauri kuwa na kapu la nishati mchanganyiko 'energy basket', yenye vyanzo vingi kuanzia mabwawa, joto ardhi, nyuklia, gesi na makaa.

Anasema ni lazima kuviboresha na kutumia njia zilizoyapa mataifa yaliyoendelea mafanikio kiuchumi bila kuogopa kuwa nchi zilizoendelea zinakataza.

Kwa wakati huu dunia inasisitiza kutumia nishati safi isiyoongeza joto duniani kama jadidifu, lakini ikumbukwe kwamba yalitumika makaa wa mawe, gesi, nyuklia na mafuta hadi kufikia maendeleo waliyo nayo leo.

"Tutumie pamoja na vile ambvyo wenzetu walitumia wakapata umeme wa uhakika kama makaa ya mawe na mafuta..." anasema DK. Byabato.

"Baba wa Taifa Ghana, Kwame Nkurumah alisema tunataka kupata uhuru wa kuamua mambo yetu wenyewe, hivyo tuangalie tusiwe watu wa kufanyiwa maamuzi ya kupata maendeleo na wenzetu wa Ulaya na Marekani."

Anashauri kutumia wataalamu na kuandaa teknolojia ya kuchakata na kupata nishati ya uhakika kwa maendeleo.

# Ndizo hasi, chanya kuendeleza demokrasia ndani ya miaka 63

**Na Sabato Kasika**

TAIFA limeanza safari nyingine ya kuelekea miaka 64 ya uhuru baada ya kumaliza maadhimisho ya miaka 63 ya uhuru yaliyofanyika juzi, kwa Watanzania kushiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii.

Jubilii ya miaka 63 ya uhuru ni ya kujivunia ikiwa na miaka mingi inayovuka nusu karne na kuna mengi ambayo nchi imepitia hadi sasa kukiwa na amani na utulivu baada ya kuwatimua wakoloni waliokuwa wameikalia Tanganyika kabla ya kuwa Tanzania.

Mafanikio mbalimbali yameonekana tangu uhuru, kama ambavyo baadhi ya wadau wa siasa wanavyoyataja, lakini pia matatizo yapo.

Ananilea Nkya ni Mwenyekiti wa Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), anaeleza kuwa nchi inapiga hatua lakini kurudi nyuma au kinyumenyume hasa kwenye kuendeleza demokrasia.

"Tunaendesha siasa ambazo zinarudisha nyuma maendeleo ya nchi, maana tunapata viongozi kwa mfumo wa siasa, hivyo tunapofanya uchaguzi unaolalamikiwa kuwa si huru na haki maana yake ni kupata viongozi wanaolalamikiwa pia," anasema Ananilea.

Mwenyekiti huyo anaongeza kuwa miaka ya hivi karibuni, Tanzania imekuwa ikifanya uchaguzi ambao wananchi wanaona kuwa haufuati utaratibu, kanuni na sheria na kwamba matokeo yake wanaochaguliwa kuongoza baadhi si chaguo la wananchi.

"Mfano mmojawapo ni uchaguzi wa serikali za mitaa uliofanyika hivi karibuni, tumesikia malalamiko na tuhuma zikihusisha baadhi ya taasisi zisizohusika kuingilia uchaguzi badala ya kuusimamia, matokeo yake wananchi na wapigakura wanalalamika." Anaeleza.

Anasema utaratibu huo wa uchaguzi unakwamisha maendeleo na kurudi nyuma na kwamba hata enzi ya uchaguzi wakati wa mfumo wa chama kimoja una unafuu kuliko hali ilivyo sasa.

Katika ufafanuzi wake anasema enzi ya chama kimoja, wananchi hawakulazimishwa kuchagua viongozi wasiowataka, walikuwa huru kuchagua mgombea au alama iliyowekwa pembeni ya picha ya mgombea katika karatasi za kura.

"Hivyo, kwa maoni yangu kuhusu hali ya kisiasa kwa miaka 63 ya uhuru, hatusongi mbele kidemokrasia tunarudi nyuma," anasema.



Ananilea Nkya



Steven Machumu



Mary Chatanda

### UTAWALA KISHERIA

Mtaalamu wa uchumi, Steven Machumu anasema Tanzania yenye amani na mshikamano, wananchi wake kwa umoja wao wameshiriki kujenga uchumi binafsi na wa taifa bila kubugudhiwa na mtu au mamlaka kwa kuwekewa mazingira wezeshi.

Pamoja na hayo, anasema tangu taifa kupata uhuru, limeendelea kusimamia haki za binadamu chini ya katiba kama zilivyoainishwa katika tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu bila kujali itikadi za vyama, dini au jinsia.

"Mimi ni mtaalamu wa uchumi, lakini kwa kuwa siasa ni uchumi, nina uwezo wa kuizungumzia. Lakini pia niseme kuwa Tanzania ni mfano kwa amani, upendo na mshikamano Afrika na pengine duniani." anasema Machumu.

Anaongeza kuwa hata mifumo huru ya utoaji haki imeendelea kuimarishwa na kuboresha kadri ya mahitaji ya jamii katika kipindi chote cha miaka 63 ya uhuru, kwa kuwa usawa mbele ya sheria umeendelea kuwapo licha ya changamoto za hapa na pale kujitokeza na kurekebishwa.

"Katika kipindi chote hicho, utawala bora wa sheria umeendelea kudumishwa, ukuaji na ujenzi bora wa utawala, sheria na demokrasia vimeendelea kujengwa kwa uangalifu ili kulinda amani ya taifa letu kutokana na uchanga wa demokrasia inayohusisha mfumo wa vyama vingi vya siasa," anasema.

Anafafanua kuwa utawala bora kwa taifa umeendelea kwa kuhusisha taasisi zote za serikali na umma kwa kuhimizwa na kutekelezwa, ingawa kuna baadhi ya taasisi hujikuta zinapoteza mwelekeo, na kwamba uwajibikaji umekuwa ukichukuliwa na kurejesha hali ya kawaida.

Vilevile, anasema taifa huru ndani ya miaka 63 limeendelea kuongeza mapambano ya kuzuia na kupambana na rushwa kama adui wa haki kwa wananchi kwa kuunda taasisi maalumu yenye kuhusika na mchakato huo.

Anaongeza kuwa Tanganyika kama taifa lililopata uhuru wake 1961 na kuungana Zanzibar mwaka 1964, muungano huo umeendelea kudumishwa kwa pande zote mbili kwa manufaa ya wananchi wote.

### MFUMO DUME MWISHO

Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT), Mary Chatanda, anasema ndani ya miaka 63 ya uhuru, mfumo dume umeendelea kupungua.

Sehemu za kazi, ndani ya vyama vya siasa, uongozi wa kisiasa na kwenye familia kuwapa nafasi za uongozi wanawake kumeonekana, anasema.

Anafafanua kuwa ingawa bado usawa wa kijinsia haujafikiwa kikamilifu, kuna dalili za kuufikia, kwa maelezo kuwa yapo mabadiliko makubwa yanayoendelea kushamiri kuanzia chini hadi juu.

"Mfano, leo tuna rais mwanamke, lakini pamoja na hayo, katika uchaguzi wa serikali za mitaa wa mwezi uliopita, wanawake waliogombea nafasi ya mwenyekiti na ujumbe wameshinda," anasema.

Bila kutaja idadi ya wanawake washindi, anasema inatia moyo kuona wanawake wanawania uongozi kwenye ngazi za vitongoji na kushinda, tofauti na miaka ya nyuma.

"Zamani haikuwa rahisi mwanamke kugombea uongozi katika kitongoji au kijiji, kwa sababu ya mambo ya mila na desturi, kwa kuamini kuwa mwanamke hawezi kuongoza, lakini sasa mtindo huo unaendelea kuwekwa kando ndani ya jamii," anasema Mary.

Hata hivyo, anasema pamoja na wanawake kupata nafasi nyingi za uongozi serikalini na katika taasisi za umma, hawapaswi kubweteka, badala yake waendelee kupaza sauti ili kufikia asilimia 50 kwa 50.

"Ni muhimu kufikia asilimia hiyo kati ya wanawake na wanaume, kwa sababu uongozi si kubeba mzigo, bali ni akili na uwezo wa kuongoza, ambavyo wanawake na wanaume wanavyo wote," anasema.

> "Ni muhimu kufikia asilimia hiyo kati ya wanawake na wanaume, kwa sababu uongozi si kubeba mzigo, bali ni akili na uwezo wa kuongoza, ambavyo wanawake na wanaume wanavyo wote.

# Baada ya kutimuliwa Syria, Assad ajisalimisha kwa Putin

• Yeye na baba mzazi walijigeuza wafalme kutawala nchi kibabe

**Na Christina Mwakangale**

BARANI Afrika mabadiliko ya kisiasa iwe kwa mapinduzi au ya mfumo rasmi kupitia upigaji kura, yamepamba moto, kuanzia Botswana hadi Senegal wananchi wamefanya 'jambo lao.'

Karne ya 21 inaweka rekodi zaidi kwa bara hili la kuleta mabadiliko ya kisiasa huku baadhi ya vyama vilivyodumu hata nusu karne vikiondoshwa madarakani.

Upepo wa mabadiliko haupo Afrika pekee na safari hii nchini Syria dunia imeshuhudia raia wakiingia, kupiga picha huku wakichukua chochote watakacho, wakidai ni kulipiza kisasi kwa miaka mingi ya ukandamizaji na umaskini kwa sababu ya Bashar al-Assad na baba yake.

Wakazi wa maeneo tofauti ni mjini Damascus wameelezea namna walivyokuwa wakisubiri kwa wasiwasi habari juu ya kile kinachotokea katika mji mkuu wa Syria usiku kucha.

Baada ya saa kadhaa za ripoti za waasi walikaribia zaidi na zaidi, vikosi vilitangaza kuwa Damascus ni 'huru' mbali na mtawala wa muda mrefu Bashar al-Assad mapema Jumapili.

Video mitandaoni kwenye vyombo vya kimataifa kama BBC, zilisambaa kwenye mitandao ya kijamii zikionyesha watu wakishangilia barabarani na kuwakaribisha wapiganaji hao waasi, pamoja na wafungwa wakiachiliwa huru kutoka katika gereza la Saydnaya.

"Hakuna mtu aliyelala nchini Syria usiku huo ... hakuna Msyria aliye ng'ambo aliyelala," Rania Kataf, ambaye anaendesha ukurasa wa Facebook wa Humans of Damascus, anasema.

"Jamii nzima ilikuwa imeshikilia simu zao zikisubiri habari za mwisho. Ninahisije? Kuzidiwa... Sote tunahisi kama tumekuwa chini ya maji, kwa miaka 13 na sote tulipumua."

"Najua kwamba kuna watu wengi ambao ni wakubwa zaidi kuliko mimi ambao wamepitia mengi sana." Anasema kwa hisia mchanganyiko, hata hivyo tangu mashambulizi ya mkundi ya waasi yaanze, lakini hakuwa na hofu tena.

Danny Makki, mwandishi wa habari anayeishi Damascus, anaelezea matukio ya Jumapili wiki iliyopita, huko Umayyad, ambako ni nyumbani kwa mashirika muhimu ya serikali, ikiwa ni pamoja na Wizara ya Ulinzi na Vikosi vya Wanajeshi vya Syria.

"Watu walikuwa wakifyatua risasi hewani, watu walikuwa wakicheza, kupiga picha na kulia," anasema mwandishi huyo.

"Nilizungumza na askari kutoka kwa wanamgambo. Mmoja anasema alikuwa akijiandaa kwa hili kwa muda mrefu. Hakuwa akishiriki katika mashambulizi ya Aleppo, lakini alipoona waasi wakiwasili viunga vya Damascus, ndipo alipochukua silaha."

Anasema baadhi ya wapiganaji hao waasi walikuwa wakitumia magari ya Jeshi la Syria yaliyotelekezwa.

"Nilipokuwa nikiendesha gari kuzunguka Damascus, niliona wanajeshi wa Syria wakitembea wakiwa katika nguo za kiraia barabarani, bila kujua wapi pa kwenda."

"Wasiwasi wa watu ulikuwa usalama, na kuhakikisha kuwa hakuna mapigano ndani ya safu ya upinzani."

"Kwa mara ya kwanza kabisa, kuna hisia za kweli za uhuru. Tunachohisi kinafanana sana na tulivyohisi wakati wa mapinduzi yalipoanza mwaka wa 2011. Huu ni mwendelezo wa ndoto ambayo ilikuwa imeanza mwaka huo."

> Wasiwasi wa watu ulikuwa usalama, na kuhakikisha kuwa hakuna mapigano ndani ya safu ya upinzani.

Mwandishi huyo anasema kuwa Wasyria wanahisi hofu na wasiwasi juu ya siku zijazo, lakini "leo, watu wote wa Syria watasherehekea tu."

Mtangazaji huyo wa televisheni ya taifa anasema viongozi wa upinzani wamehakikisha usalama wa vituo vya kijeshi vya Russia na balozi za kidiplomasia katika eneo la Syria.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Russia, inasema kuwa kambi hizo nchini Syria zimewekwa katika hali ya tahadhari, lakini inadai kuwa hakuna tishio kubwa kwao kwa sasa.

## NANI ANAMSHTAKI ASSAD

Bashar al-Assad alikuwa mshirika mkuu wa Russia katika Mashariki ya Kati. Kremlin au ikulu ya Urusi ilikuwa imewekeza sana kwake.

Mamlaka ya Russia, ikajitahidi kukubali kupinduliwa kwake lakini kama pigo kubwa kwa upande wa Moscow.

Siku ya Jumapili usiku kipindi cha televisheni cha taifa cha Russia cha kila wiki kililenga jeshi la Syria, kikililaumu kwa kutopigana dhidi ya waasi.

"Kila mtu aliweza kuona kwamba hali ilikuwa inazidi kuwa mbaya kwa mamlaka ya Syria," mtangazaji Yevgeny Kiselev akasema.

"Lakini huko Aleppo, kwa mfano, maeneo yaliachwa bila vita vyovyote. Maeneo yenye ngome yalisalimishwa moja baada ya jingine na kisha kulipuliwa, licha ya wanajeshi wa serikali kuwa na vifaa bora zaidi na kuwazidi washambuliaji mara nyingi. Inashangaza."

Mtangazaji huyo anadai kwamba Russia, daima ilikuwa na matumaini ya upatanisho nchini Syria.

"Bila shaka hatujali kile kinachotokea Syria. Lakini kipaumbele chetu ni usalama wa Russia yenyewe, kile kinachotokea katika ukanda wa Operesheni Maalum ya Kijeshi (vita vya Urusi nchini Ukraine)."

Licha ya miaka tisa ya Russia, kumwaga rasilimali katika kumweka Bashar al-Assad madarakani, Warusi, wanaambiwa wana mambo muhimu zaidi ya kuhangaikia, si jambo lake.


Rais wa Syria aliyepinduliwa, Bashar al-Assad. **PICHA: DW**

## ALIKO SASA

Rais huyo aliyepinduliwa yuko Moscow na familia yake baada ya Urusi kuwapa hifadhi kutokana na sababu za kibinadamu.

Jumapili usiku na ikulu ya Kremlin, ilisisitiza kuwa makubaliano yamefikiwa, ili kuhakikisha usalama wa kambi za kijeshi za Urusi nchini Syria.

Awali Moscow ilisema kambi hizo ziko katika tahadhari kubwa lakini hakukuwa na kitisho dhidi yao kwa sasa. Assad ameikimbia nchi baada ya waasi kuchukua udhibiti wa mji mkuu Damascus huku akitoa maagizo kwamba ukabidhi wa madaraka ufanyike kwa amani.

Rais wa Marekani, Joe Biden, anasema ni lazima Assad awajibishwe kwa vitendo vya mauaji na mateso kwa mamia ya maelfu ya Wasyria. Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa litafanya hivi leo mkutano wa dharura na wa faragha ili kuijadili hali inayoendelea nchini Syria.

## ASSAD

Bashar Hafez al-Assad, ana miaka 60 akizaliwa Septemba 11, mwaka 1965, akiwa mwanasiasa wa Syria ambaye aliyeanza kuongoza taifa hilo Julai 17, 2000.

Alikuwa kamanda mkuu wa Jeshi la Siria na Katibu wa Mkoa wa tawi la Chama cha Waajemi la Ba'ath nchini Syria, baba yake, Hafez al-Assad, alikuwa Rais wa Syria kutoka mwaka 1971 hadi 2000. **BBC**





# Familia zaonywa kugeuza wenye ulemavu kitega uchumi

**Na Peter Mkwavila,** BAHI

SERIKALI imezionya familia zenye watu wenye ulemavu kuacha tabia ya kuwatumia kitega uchumi kwa kuwazungusha mitaani kuomba fedha.

Onyo hilo lilitolewa na Katibu Tawala wa Wilaya ya Bahi, Sarah Ngalingasi kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule kwenye Kongamano la Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Watu wenye ulemavu yaliyofanyika kimkoa wilayani hapa.

Sarah, alisema kuwa kuna familia zinawatumia watu wenye ulemavu kama sehemu ya kitega uchumi kwa kuwazungusha mitaani na kuwaweka barabarani kuomba fedha na kuwaondolea hadhi ya utu wao.

"Jamii inatakiwa kutambua wazi kuwa ulemavu siyo umaskini au kuondolewa hadhi ya utu, bali mtu mwenye ulemavu anatakiwa kuthaminiwa na kupewa haki yake kama alivyo kwa watu wengine wasiokuwa na ulemavu," alisema.

Sarah, alisema baadhi ya wazazi, walezi wenye watoto wenye ulemavu, nao wamekuwa wakiwatumia vibaya badala ya kuwapatia haki yao ya msingi ya kuwapeleka shule.

Alisema lazima watambue watu wenye ulemavu wanatakiwa kupata haki zao za msingi na siyo kuwatumia kama tiketi kuwa ombaomba wa mitaani na barabarani.

Katibu Mkuu wa Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu nchini (SHIVYAWATA) Taifa, Jonas Lubago aliwataka watu hao wenye ulemavu kujiamini na kujitambua ili waweze kupatiwa fursa ikiwamo uongozi na kupatiwa mikopo kwa ajili ya kuanzisha miradi ya ujasiriamali.

Lubango, aliiomba serikali kuboresha miundombinu ya watu wenye ulemavu na kuwawekea wakalimani.

# Singida kupata mabilioni kwa vichaka na misitu

**Na Waandishi Wetu**

WILAYA za Manyoni na Ikungi mkoani Singida zinatarajia kuanza kupokea mabilioni ya fedha kwa utunzaji wa misitu ya asili na vichaka adimu vya Itigi duniani na Bara la Afrika vinavyopatikana nchini na Zambia.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, aliyasema hayo juzi wakati wa Maadhimisho ya 63 ya Uhuru wa Tanganyika. Katika maadhimisho hayo viongozi wa chama, serikali na wananchi walisherehekea kwa kupanda miti 501 katika Hospitali ya Rufani ya mkoa huo.

Dendego, alitaja mkakati mwingine ni kutengeneza mpango wa matumizi ya ardhi, kuendelea kuhifadhi misitu ya asili ambayo ni fedha kutokana na biashara ya hewa ukaa kuuingizia nyingi na mkoa huo.

"Wilaya yetu ya Manyoni na Ikungi ipo mbioni itaanza kupokea mabilioni ya fedha muda mchache ujao, niwapongeze wakuu wa wilaya kwa kupamabana maana wananchi wetu wakiona kitu ndio wataamini, miti yetu ni dhahabu ya kijani," alisema.

Alisema mkoa huo utaendelea kuhamasisha upandaji miti na kwamba uzinduzi rasmi utafanyika mwanzoni mwa mwakani na kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia ya gesi ili kunusuru misitu kukatwa ovyo.

Katika hatua nyingine, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amewataka wananchi kuendelea kutunza mazingira kwa kupanda miti kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi na kuimarisha ukanda wa kijani.

Akizungumza na wakazi wa mji wa Dodoma Kata ya Makutupora kwenye maadhimisho hayo, alisema kila mmoja ana wajibu wa kuhifadhi mazingira kwa kupanda mti wa kivuli na matunda kwenye maeneo yao.

Mtendaji Mkuu wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Profesa Dos Santos Silayo, alisema wataanza kutoa utaalamu nchini wa kupanda miti ili kuwe na misitu ya mijini na kuifanya Tanzania kuwa ya kijani.

Nao watumishi wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Benjamin Mkapa wametoa zawadi kwa watoto waliozaliwa kabla ya wakati maarufu kama njiti ili kukua na kutimiza siku zinazotakiwa kitaalamu.

Mkurugenzi Mtendaji wa BMH, Profesa Mabele Makubi, alisema: "Tumeadhimisha Siku ya Uhuru kwa kufanya usafi na kutoa zawadi kwa watoto waliozaliwa kabla ya muda. Huu ni upendo tumeonyesha kwa wagonjwa wanaokuja BMH kupata matibabu."

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Watoto, Julieth Kabengula, alisema hospitali hiyo ni kimbilio kuokoa maisha ya watoto hao wanaozaliwa kabla ya wakati .

"Kwa kawaida ndani ya mwezi, wastani wa watoto wanaozaliwa kabla ya wakati 35 hadi 40 wanapokelewa na kuhudumiwa na mpaka sasa tumepokea mtoto mwenye gramu ndogo 600 na tumehakikisha anapata matibabu hadi kuruhusiwa," alisema.



Taka zikiwa zimetupwa na kutelekezwa bila ya kuondolewa kwa muda mrefu kando ya barabara eneo Malamba Mawili, Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shirika laja na usawa kwa wanawake, wanaume

**Na Paul Mabeja,** CHAMWINO

SHIRIKA la Action Aid Tanzania limezindua Mradi wa Transformative Impact Fund (TIF) kuhamasisha jamii kutoa fursa sawa kwa wanawake na wanaume kuwa na haki ya kumiliki.

Akizungumza jana mjini hapa, Mratibu wa Mradi huo, Happy Itros, alisema unatekelezwa katika nchi za Rwanda, Burundi, Tanzania na Jamhuri ya Demokrasia Kongo (DRC).

"Huu mradi kwa Tanzania upo mikoa miwili Dodoma na Singida katika wilaya ya Chamwino vijiji vya Mlowa Barabarani, Mloda, Nzali, Kawawa, Msanga, Iringa Mvumi, Makang'wa, Chinangali II, Chamwino na Mahama," alisema.

Alisema wanahamasisha jamii kubadili mtazamo hasi wa kuwanyia wanawake fursa ya kumiliki ardhi kama ilivyo kwa wanaume.

Alisema jamii bado ina mtazamo hasi wa kuwanyima wanawake fursa ya kumiliki ardhi kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo mila na desturi potofu.

Vilevile, alisema mradi huo una lenga kuwawezesha wakulima kupaza sauti za changamoto zao kwa kushiriki kutengeneza suluhisho kupitia majukwaa ya kijamii, kuchanganua sera na mipango itakayochangia kilimo ikolojia.

Mratibu wa Actionaid Tanzania, Samwel Mesiak, alitaja sababu zinazochangia wanawake kutomiliki kuwa ardhi ni mila, desturi na imani potofu tangu enzi za mababu.

"Mwaka huu tumekuja na kampeni yetu yakusema mwanamke kumiliki ardhi ni haki yake na tupambane kikamilifu kuhakikisha tunafungua fursa za wanawake kumiliki ardhi, ukatili wa kijinsia haumaanishi tu kupiga mke, kumpiga mume au kumnyima chakula lakini pia kwenye sekta ya uchumi," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya Wanawake wa Kijiji cha Mloda, Mhazini wa Jukwaa la Wakulima Wanawake Wadogo Wilaya ya Chamwino (JUWACHA), Nuru Mpanda, alisema mwanamke na mwanaume wananafasi ya kumiliki ardhi.



# TBT kuwekeza viwanda vya teknolojia ya kisasa

**Na Halfani Chusi**

BODI ya Chai Tanzania (TBT) imetangaza mpango wa kuwekeza katika viwanda vya teknolojia ya kisasa na kupunguza gharama za uzalishaji wa chai na kuongeza thamani ya zao hilo.

Mpango huo ulitangazwa jana na Kaimu Mkurugenzi wa Bodi hiyo, Beatrice Banzi katika kikao na ujumbe wa watu watano kutoka Japan baada ya kuwasikili nchini kujifunza na kubadilishana uzoefu katika kilimo cha chai.

Ugeni huo, uliowasili nchini Desemba 7, utakuwapo hadi Desemba 14 na kufanya ziara ya kutembelea mashamba ya chai nchini yakiwamo ya mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ya Njombe na Mbeya.

Katika kikao hicho kilichofanyika katika ofisi za bodi hiyo jijini Dar es Salaam, Beatrice, alisema wamejifunza kutoka kwao jinsi ya kurahisisha kilimo kwa kutumia teknolojia za kisasa.

"Tumeona wao wanasema hawana nguvu kazi ndipo wakaanza kubuni jinsi ya kufanya kazi za shambani bila watu kwa kutumia mapinduzi ya viwanda," alisema na kuongeza:

"Na sisi tunachokitarajia baada ya kikao hiki, ni mapinduzi ya viwanda kwa sababu wao hawana nguvu kazi sisi tunayo, lakini mitaji ya kuwalipa inakuwa shida kwa hiyo ni vizuri kutumia viwanda vyenye teknolojia ya kisasa ambavyo vitasaidia kupunguza gharama katika uzalishaji wa chai kama wanavyofanya wao."

Kwa mujibu wa Beatrice, matarajio yao kutoka kwa ugeni huo mbali na mapinduzi ya viwanda ni kuongeza ubora wa chai inayozalishwa nchini na kukabiliana na ushindani katika soko la dunia.

Akizungumza kwa niaba ya Balozi wa Tanzania nchini humo, Baraka Luvanda, Edna Chuku, alisema ugeni huo una umuhimu mkubwa kwa taifa.

Edna aliyeambatana na ugeni huo, alisema una umuhimu kwa sekta ya chai nchini kwa kuwa umekuja na kampuni mbili kubwa za chai kutoka Japanza Kawasaki Kiko na Nasa Cooperation.

"Ujio wa ugeni huu utaleta matukio chanya kwa sababu wameonesha nia ya dhati ya kuwekeza Tanzania katika Sekta ya Chai, ukizingatia kwao hawana nguvukazi kubwa na uzalishaji wao ni mdogo kutoka na jiografia yao kwa hiyo wanatafuta masoko kutoka nchi mbalimbali moja wapo ikiwa Tanzania " alisema Edna ambaye ni Mratibu Masuala ya Uchumi Ubalozi huo.

Menaja Masoko Bodi hiyo, Selemani Chillo, alisema upande wa masoko ya chai hali inazidi kuimarika na kuwa nzuri siku hadi siku na kwamba tayari wamefungua soko jingine nchini Oman.

Chillo, alisema wiki ijayo wanatarajia kwenda Saud Arabia kufungua soko jingine mahususi kwa nchi za Uarabuni.

Mwakilishi Kutoka Kampuni ya Nasa Cooperation, Gaelle Lagrouas alisema amefurahi kuja nchini na kuona fursa kubwa za zao la chai na kuahidi kushirikiana na bodi hiyo kukuza soko la zao hilo.

Ujio wa ugeni huo nchini ni matokeo ya ziara ya bodi hiyo nchi Japan Julai mwaka huu.

# Serikali yashauriwa kuwatafutia wakulima masoko

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

SERIKALI imeshauriwa kuhakikisha wakulima wanapata soko la uhakika la mazao baada ya mavuno.

Ushauri huo ulitolewa juzi na Katibu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Mkoa wa Njombe, Baraka Kivambe wakati akizungumza na Nipashe katika Maadhimisho ya miaka 63 ya Uhuru wa Tanganyika.

Kivambe, alisema wakati maadhimisho hayo yakifanyika juzi, serikali ina wajibu wa kuhakikisha wakulima wanapata soko la uhakika la mazao yao hususani mahindi ili wazalishe kwa tija.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Njombe, Justin Nusulupila, alisema mafanikio yamepatikana katika sekta za afya, elimu, nishati, kilimo na miundombinu.

Nusulupila, aliwataka wanasiasa kudumisha amani kwa kutotoa lugha za chuki ili nchi ibaki salama.



Mratibu wa Taasisi ya Wanawake na Samia Wilaya ya Ilala, Upendo Mwakwenda (kulia), akikabidhi msaada wa vitu mbalimbali kwa baba mlezi wa kituo cha kulelea watoto yatima cha Kind Heart Afrika, Issa Kimati (kulia), Chanika Kigezi, wilayani humo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Wanaoharibu miti kukiona

**Na Elizabeth John,** WANGING'OMBE

SERIKALI wilayani hapa Mkoa wa Njombe imeonya haitawafumbia macho wananchi watakaoharibu miti inayopandwa katika kampeni ya kutunza mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Onyo hilo lilitolewa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe, Zacharia Mwansasu wakati Kongamano la Kumbukizi ya Miaka 63 ya Uhuru lililofanyika katika Kata ya Wanging'ombe na upandaji wa miti zaidi ya 900.

Mwansasu, alisema miti hiyo imepandwa katika kata 21 zilizopo wilayani hapa ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi.

"Nawaomba Watanzania wote kuenzi na kutambua jitihada za serikali yetu katika kupeleka maendeleo kwa wananchi wake baada ya uhuru," alisema.

Alisemani fahari kuendeleza jitihada za viongozi na waasisi wa taifa la Tanzania kwa kuwa mstari wa mbele kutunza, kuhifadhi mazingira na rasilimali zilizopo nchini.

Mwansasu, alitumia fursa hiyo kumshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuiongoza nchi kwa amani na utulivu.

Diwani wa Kata ya Wanging'ombe, Geofrey Nyagawa, alisema wilaya yao imechangia harakati za uhuru ikiwa na historia ya kuwa na uanzilishi wa Chama cha TANU miaka ya 1954-55 katika Kata ya Udonja.

Mhifadhi kutoka Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) Wanging'ombe, Abdu Mnjokava, alisema miche ya miti 5,000 ya aina mbalimbali ikiwamo mdodoma, mivengi na parachichi imepandwa katika wilaya hiyo.

"Lengo ni kuendelea kuhifadhi na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi yanayoendelea kuleta athari mbalimbali hapa duniani," alisema.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala la Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), (Afya), Dk. Festo Dugange ambaye ni Mbunge wa Wanging'ombe alitoa rai kwa wananchi kutunza mazingira kwa kupanda miti katika maeneo yao.

# Kituo chaomba msaada wa magodoro, vitanda

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

SERIKALI na wadau nchini wameombwa kutoa msaada wa vitanda na magodoro kwa wagonjwa wa kituo cha tiba ya asili cha uungaji mifupa kilichopo Kijiji cha Itunduma Halmashauri ya Wilaya ya Njombe mkoani hapa.

Ombi hilo lilitolewa juzi na Mtaalamu wa Tiba za Asili, Dk. Deo Thomas wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake.

Dk. Thomas, alisema amejenga majengo ya kulaza wagonjwa katika kituo hicho kilichoko eneo la Wangama, lakini hakina vitanda na magodoro.

"Mtu akija akavunjika mkono namtibu kwa siku 10 hadi 15 na mguu siku 25 na anaanza mazoezi na kwenda nyumbani, naomba tu msaada kwa serikali na wadau ili nipate sehemu nzuri ya kuwalaza wagonjwa wangu," alisema.

Dk. Thomas, alisema anatibu miguu na mikono iliyovunjika kwa kutumia majani ya miti shamba kwa kuchua hadi kuunga.

"Natumia miti na majani ya kawaida kuchua na hii miti ina nguvu kubwa sana, nikimpaka mtu hata kama mishipa imepanguka unasikia yenyewe inajipanga bila ya kunyooshwa," alisema. Alitoa rai kwa jamii kuacha kukata miti ya asili na kupanda ya kisasa kwa sababu wanapoteza dawa.

Dk. Thomas, alisema tiba za asili zimekuwa na msaada kwa jamii na kuwataka serikali na wadau kuzithamini na kuunga mkono kwa sababu wanasaidia kuokoa maisha ya watu.

Baadhi ya wagonjwa wa kituo hicho, walisema walikwenda kupata huduma wakiwa wamekata tamaa kutokana na kuvunjika vibaya mifupa ya mikono na miguu.

Mmoja wa wagonjwa hao, Agrey Nyagawa, alisema alipata ajali ya gari na kuvunjika mfupa mara nne na anaendelea vizuri baada ya kupata huduma nzuri.

Daudi Kinyamagoa, alisema alivunjika mguu kwa kuanguka, tiba aliyoipata kwa kipindi cha wiki moja imesaidia na sasa anaweza kukanyaga chini.





# ACT yajipambanua ajira nchini

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema siyo wakala wa ajira nchini bali kimebeba jukumu la kupigania haki na maendeleo ya watu wote nchini kwa maslahi ya Taifa.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki iliyopita na Mwenyekiti wake, Othman Masoud Othman, wakati akifungua Kongamano la Kitaifa la Vijana wa ACT-Wazalendo Mkoa wa Kati Kichama lililofanyika Dunga Mkoa wa Kusini Unguja.

Othman ambaye ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, alisema utajiri na rasilimali zilizopo zinaweza kuwainua vijana kiuchumi na miundombinu duni ya uongozi bora inayodhoofisha azma hiyo na kuifanya nchi kuendelea kuwa na idadi kubwa ya wategemezi.

Akizungumzia kuhusu kura ya siku mbili Zanzibar, alisema kuwa: "Wajibu wetu ni kuilinda Katiba ya Zanzibar kama ambavyo tuliahidi katika kiapo kupambania haki na kuwahudumia wananchi, tunaahidi 'Kura ya Mapema' haitojirudia Zanzibar."

Othman, alisema chama hicho kiliahidi muda utakapowadia mwaka 2025, kitaendesha nchi kistaarabu na amani ili kuvutia wawekezaji kuzalisha nafasi nyingi za ajira kwa vijana nchini na kuondoa janga la ukosefu wa ajira kwao.

Alisema iwapo kutakuwapo viongozi wenye maono ni rahisi zaidi kuleta mafanikio ya kiuchumi nchini.

"Chama siyo wakala wa ajira kama wafanyavyo vyama vingine, bali dhima yake kuu ni kupigania haki na maslahi ya watu wote bila ya ubaguzi," alisema Othman.

Aliwataka vijana kuacha kughilibiwa kwa kivuli cha kupewa ajira na badala yake wasimame imara kutekeleza dhamira ya kuitafuta Zanzibar yenye mamlaka kamili.

Wakitoa salamu zao, Katibu wa Taifa wa Vijana na Mwenyekiti wa Ngome ya Vijana Mkoa wa Kichama wa Kati wa chama hicho, Muhamed Khamis Busara, na Suleiman Ali Seif kwa nyakati tofauti, walisema 2025 ni mwaka wa maamuzi na wa mabadiliko.

Walisema ni wajibu wao kuwa mstari wa mbele kulifanikisha hilo.

Kongamano hilo ambalo ni mwendelezo wa Makongamano ya Ngome ya Vijana yanayoendelea nchini kote, lilibeba Kaulimbiu ya "Nafasi ya Vijana kuelekea Uchaguzi 2025 na Ukombozi wa Zanzibar".

Kongamano hilo ambalo limeshuhudia mjadala wa "Ni Upi Wajibu wa Vijana kwenye Uchaguzi wa 2025 katika Kupigania Zanzibar yenye Mamlaka Kamili", lilifungwa na Mwanasheria Mkuu wa ACT-Wazalendo, ambaye ni Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Omar Said Shaaban.

## Viongozi wahimizwa kuleta maendeleo Z'bar

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, amewataka viongozi wa Serikali ya Zanzibar kisiwani Pemba kuongeza kasi ya uwajibikaji ili kumsaidia Rais Dk. Hussen Mwinyi kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar.

Abdulla alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki iliyopita katika kikao kazi kilichowashirikisha wakuu wa mikoa na wilaya, maofisa wadhamini na wakurugenzi wa mabaraza ya miji, manispaa na halmashauri.

Alisema azma ya serikali ni kuhakikisha inawaletea wananchi maendeleo kwa kuwafikishia huduma bora na stahiki katika maeneo na kutatua changamoto zinazowakabili.

Abdulla, aliwahimiza kufanya kazi kwa ushirikiano, kusaidiana na kupeana maelekezo chanya ili kufikia malengo ya kuwaletea wananchi maendeleo.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), Massoud Ali Moh'd, aliwataka viongozi hao kuelekeza nguvu zao kuitumikia serikali ili kutimiza malengo yake iliyojiwekea ikiwamo kuwaletea wananchi maendeleo.

Wakati huo huo; Makamu huyo wa pili wa rais, Abdulla, amefanya ziara ya ukaguzi wa ukatarabati wa uwanja wa Gombani ikiwa ni maandalizi ya sherehe za Miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar zitakazofanyika mwakani.

Akizungumza na makandarasi wanaojenga uwanja huo, aliwataka kufanya kazi usiku na mchana ili kuhakikisha unakamilika kwa wakati uliopangwa na ubora wa hali ya juu ili kudumu kwa muda mrefu.

Mshauri Elekezi Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA), Said Malik, alisema wamepokea maelekezo hayo na kuahidi kufanya kazi usiku na mchana ili ujenzi ukamilike kwa wakati.



Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Rais mstaafu Dk. Jakaya Kikwete, akionesha kampasi itakavyokuwa, wakati wa ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa mradi katika Taasisi ya Sayansi za Bahari, kampasi ya Buyu, iliyopo kusini mwa Mji Mkongwe wa Zanzibar, mwishoni mwa wiki. **PICHA: ISSA MICHUZI**

# Ujenzi taasisi wamkuna JK

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUU wa Chuo Kikuu cha Bahari Dar es Salaam, Dk. Jakaya Mrisho Kikwete amesema kukamilika kwa ujenzi wa taasisi ya sayansi za bahari ya chuo hicho utaleta maendeleo makubwa ya elimu kwa wanafunzi wa Tanzania.

Dk. Kikwete alitoa kauli hiyo wakati wa ziara ya kukagua ujenzi wa Mradi wa Heet wa Taasisi ya Sayansi za Bahari ya chuo hicho unaoendelea eneo la Buyu visiwani hapa.

Alisema taasisi hiyo ina lengo la kutoa ushindani wa elimu kwa wanafunzi wa ndani na nje ya Tanzania na kupata wataalamu bora waliobobea.

"Chuo hiki kina umuhimu mkubwa kwa maendeleo ya elimu kwa wanafunzi wa Tanzani ni vizuri kuwapo na kuendelezwa," alisema.

Kikwete ambaye Rais mstaafu wa Tanzania, alisema taasisi hiyo ina umuhimu mkubwa katika utafiti, teknolojia na matumizi ya rasilimali za bahari na inatarajiwa kuwa kituo bora kwa wataalamu wa sayansi za bahari barani Afrika.

Alisema uwekezaji katika elimu na utafiti ni njia bora ya kuhakikisha maendeleo endelevu na ushindani wa kimataifa kwa maendeleo ya taifa kulingana na wakati wa sasa.

"Kwa vile dunia inakwenda na wakati na Tanzania ni sehemu ya dunia hiyo, lazima kujipanga kuelekea huko," alisisitiza.

Alisema taasisi sayansi za bahari ina muhimu mkubwa kwa vijana kujifunza tafiti za viumbe vya baharini kwa maji ya chumvi na baridi katika wakati huu ambao nchi ipo katika uchumi wa buluu.

Kikwete, alisema ili kufikia mafanikio ya taasisi hiyo, wasimamizi wa chuo hicho lazima kuipanga zaidi kufundisha tafiti ili kuwa na wataalamu waliobobea katika masuala ya bahari.

Akizungumzia kuhusu ujenzi huo, alisema ulikwama kwa miaka 20, hivyo wakaamua kuufufua kupitia Heet wa mkopo kutoka Benki ya Dunia (WB) kwa kuomba mkopo wa dola milioni nane ili kumaliza na kuwapa fursa vijana wa watanzania kujifunza mambo mbalimbali kuhusu bahari na rasilimali zake.

Alisema serikali imejipanga kuhakikisha vijana wanapata elimu ili kuwa na wataalamu wa baadaye.

"Serikali imejipanga kuhakikisha vijana wake wanapata elimu ili kuwa na wasomi wazuri wa baadaye na hiyo ndiyo target (lengo) yake," alisema.

Naibu Mratibu wa Mradi huo, Dk. Liberato Haule, alisema Shilingi bilioni 11.1 zitatumika hadi kukamilika kwake.

Alisema ujenzi huo ambao hadi sasa umefikia asilimia 90.

Alisema kwa sasa chuo hicho kina uwezo wa kuchukua wanafunzi 139 kati ya 280.

"Tunafahamu umuhimu wa elimu ndiyo maana malengo yetu katika mradi ni kufikia wanafunzi wengi zaidi ili kupata taaluma," alisema Dk. Haule.

Mshauri wa michoro wa mradi huo, Fatma Mhammed, alisema ujenzi wa mradi umezingatia uimara wa jengo kuendana na wakati wa sasa.

# Mbowe, Lissu wavunja ukimya

**Na Elizabeth Zaya**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe na Makamu wake, Tundu Lissu, wamejitokeza kwa pamoja mbele ya waandishi wa habari, wakitolea ufafanuzi mambo mbalimbali, kikiwamo kinachodaiwa "msuguano kati yao".

Kukiwa na tetesi za Lissu kumkabili Mbowe katika uchaguzi ujao ndani ya chama, Mwenyekiti huyo amesisitiza hataondoka wala kustaafu kupigania chama hicho mpaka anaingia kaburini.

Mbowe alitoa kauli hiyo jana katika mkutano na waandishi wa habari kutangaza uamuzi wa Kamati Kuu ya chama hicho iliyokuwa imejifungia kwa siku kadhaa kujadili yaliyojiri kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Alisema watu wawe na subira kwa kuwa mambo yako jikoni yanapikwa kuhusu kugombea au kutogombea tena nafasi ya mwenyekiti wa chama, akiwapiga kijembe wanaomtaka apumzike nafasi hiyo, akidai kwamba hajamzuia mtu kugombea nafasi yoyote ndani ya chama hicho.

"Na anayesema Mbowe anagombea mwenyewe, kanionea, sijawahi kugombea mwenyewe, wala kumzuia mtu yeyote kugombea," alisema Mbowe.



Mwenyekiti CHADEMA, Freeman Mbowe



Makamu Mwenyekiti CHADEMA, Tundu Lissu

Alisema chama hicho hakijawahi kuwa na utaratibu wa kutoa nafasi moja wa kugombea ya mwenyekiti bali hutoa nafasi kwa yeyote anayejisikia kugombea, kufanya hivyo.

"Si msubiri tu muda useme, shida iko wapi, ingekuwa kutokusema kwangu nimemzuia mtu yeyote asiseme, hilo ni jambo lingine.

"Vitu vingine vinapikwa ndani jamani, viacheni vipikwe viive, wengine wanasema 'mbona umekaa sana miaka 20...?' Hiyo ni mia-ka ya kukomaa... wewe jaribu kukomaa kwa miaka 20 ufanye kazi yangu uone ndani yake utakavyojutia," alisema Mbowe.

"Mwingine analinganisha kwamba hata Mwalimu Julius Nyerere (Rais wa kwanza wa Tanzania), aling`atuka... Nyerere alikuwa mtumishi wa umma wa nchi, analipwa mshahara, marupurupu, hafungwi, hashtakiwi, hanyang`anywi mali, anatukuzwa, anaishi kwenye nyumba za umma, sisi wana CHADEMA unavyotuona hapa, wote hawa wanajitolea," alisema.

Mbowe aliendelea kueleza: "Hii kazi nimeipigana miaka 33 bila kupumzika na sina mpango kabisa wa kuacha ngoma hii, na ninaposema mimi ninapigana, haina maana na wenzangu nao wasipigane, tunapigana wote, hatutaki biashara ya kustaafu siasa wakati uonevu, ukandamizi, utapeli katika siasa yetu unaendelea.

"Tunapumzikaje? Kwani tumeyapata yale tuliyokuwa tunayapigania? Tutapambana mpaka siku ya kuingia kaburini bila kujali wewe ni mwenyekiti, katibu au mbunge. Kazi ya kudai haki katika taifa letu haipaswi kuwa ya muda.

"Unaniambia nikastaafu... tunayoyapigania yametimia? Hivi tungekuwa tunalipwa kodi na wananchi mngesemaje? Mapenzi yote kwa nchi hii, mnawaambia wastaafu, yaani mimi Mbowe nimechoka?" alihoji.

### MIVUTANO NA LISSU

Mbowe alifafanua kuhusu kinachotajwa mivutano yake na Lissu, akisema: "Mimi nimekaa na Lissu hapa, watu wanasema 'wamekaa eeee...' mtasubiri sana, mambo ya kugombea au kutokugombea si 'issue'... 'issue' tunajenga nyumba moja, tunabebaje fito zetu kwenda kwenye malengo yetu?

"Watu wanasema Makamu wangu anapigwa vita, inawezekana anapigwa vita... mimi je, wote tunapigwa vita... Mbowe anapigwa vita, Lissu anapigwa vita, Mnyika anapigwa vita, vivyo hivyo na watu wetu wanapigwa vita, na wanaopiga vita wala siyo wana-CHADEMA."

Katika hilo, Lissu alisema: "Mimi ninatembea na risasi mgongoni, nitaogopa mawe ya mitandaoni, niliwahi kuitwa mhaini na kiongozi wa serikali (anamtaja), sasa nitaogopa mashujaa hawa wa mitandaoni?"

Kuhusu maridhiano na serikali, Mbowe alisema waliingia katika maridhiano kwa sababu waliamini kauli za viongozi wa nchi zingefanyiwa kazi.

"Sasa wasipotekeleza si dhambi yangu... mimi niliamini kauli ya viongozi ambao waliitoa hadharani na ndio maana huu uchaguzi (wa serikali za mitaa) turishiriki, tumeshiriki na tumeona wapi panavuja," alisema.

Mbowe pia alisema chama hicho kimejipanga kuzuia kufanyika kwa Uchaguzi Mkuu mwakani endapo hakutafanyika mabadiliko katika mfumo mzima wa usimamizi wa uchaguzi huo.

Katika hilo, Lissu alisema: "Tunaposema 'no reforms no election', haimaanishi kususia, la hasha! Inamaanisha kuzuia uchaguzi, ni kwa namna gani... tujiandae!

"Mfumo mzima wa usimamizi wa uchaguzi hauko huru, uandikishwaji wapigakura, mfumo mzima wa uteuzi wa wagombea, mfumo mzima wa kampeni, masuala yote yanayohusu mawakala, masuala yote yanayohusu siku ya uchaguzi yenyewe, yote ni matatizo matupu."

*Kwa maoni; +255 677 020 701*
*Email; costumerrelations@guardian.co.tz*

---


KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA
WILAYA YA KARATU

UTHIBITISHO WA MSIMAMIZI WA MIRATHI

SHAURI LA MIRATHI NO. 30239 LA MWAKA 2024

MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIZI WA MIRATHI YA

ROZINA GREGORY BAHA..........................MAREHEMU

MONICA PETER TSORAY..........................MWOMBAJI

TAARIFA YA KAWAIDA
(KANUNI YA 75)

Watu wote wanaodaiwa kuwa na haki katika Mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia maombi haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa barua ya usimamizi wa mirathi kwa mwombaji aliyetajwa hapo juu mapingamizi yote kuhusu maombi haya yawe yameandikwa mnamo au kabla ya tarehe 19 DECEMBA, Mwaka 2024

Imewasilishwa Karatu leo tarehe 28 mwezi NOVEMBER, Mwaka 2024

S.S.MUSHUMBUSI
HAKIMU MKAZI MKUU
MAHAKAMA YA WILAYA KARATU



KUPOTEA KWA CHETI



**NASSANIA ELIAS NDINGA,** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI CHA KIDATO CHA NNE CHENYE NAMBA YA USAJILI **NS3661|0046** KILICHOTOLEWA NA YA SHULE YA BEROYA SECONDARY SCHOOL-SONGEA RUVUMA MWAKA 2016, KWA YOYOTE ATAKAEKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/MBE/MBE/40726/2024.**



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA

Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE

Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM

Usimamizi wa mirathi Na 1859 / 2024

KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA
MAREHEMU MURSALI MOHAMEDI ISERE WA MACHINJIONI A

KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI
YALIYOLETWA NA SUDY MURSALY ISSERE

TANGAZO
(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 12 Mwezi 12 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika

Imetolewa leo Tarehe 18 Mwezi 11 Mwaka 2024

HAKIMU



KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ZENA HASHIMU KINGAZI,** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 208 BYD.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/KIL/HAI/29897/2024.**



DEEP POLL ON CHANGE OF NAME
(Under Cap 117)
The Registration of Documents Act

A. DECLARATION
By this deed, **I ALLY MOHAMED KAGIR**I of 0684740736, a resident of Arusha Regions, DOTH HEREBY absolutely renounce relinquish and abandon the use of my former names of **ALI MOHAMED KAGIRI** and **ALLY M KAGIRI** and in lieu thereof assume and adopt the name, **ALLY MOHAMED KAGIRI** and in pursuance of such change of the name as aforesaid I **HEREBY DECLARE:-**

1. That both referred names are mine and the documents they appear are all mine and genuine
2. That I shall at all times thereafter in all records, deeds and instruments, in writing and in all actions and proceedings and upon all occasions whatsoever use and sign the said name, **ALLY MOHAMED KAGIRI.**

B. REASONS
3. A reason for changing the said name is to bring uniformity and consistency. In my child's bithcerticate which bear the name **ALLY MOHAMED KAGIRI,** however academic certicatesbear the name **ALLY M KAGIRI** and in my National Identity Card bear the name **ALI MOHAMED KAGIRI.** These differences have occasioned some difficulties in accessing some services and for the interest of consistence and avoidance of any confusion I made this declaration.

C. AUTHORIZATION
4. **AND I HEREBY** expressly authorize and require every person whatsoever at all times after the date stated below, describe and address me by the adopted name of **ALLY MOHAMED KAGIRI**

D. VERIFICATION
5. **I, ALLY MOHAMED KAGIRI DOTH HEREBY** verify that, all that I have stated above in declaration, reasons and authorization are true to the best of my knowledge.

Verified at Arusha this.......17th...... day of October, 2024.

DEPONENT

IN WITNESS THEREOF, I have unto subscribed my name ofALLY MOHAMED KAGIRIon the day and manner hereinafter appearing.

SIGNED and DELIVERED by the said
ALLY MOHAMED KAGIRI
Who is personally known to me.
This ...17th...October, 2024

DEPONENT



BEFORE ME:
Name: ...
Signature: ...
Address: ...P.O. Box 16081...
Qualification: Commissioner for Oath



IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA

PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 29640 OF 2024

In the Matter of the estate of the late of MARTHA CHRISTOSIA MINJA of MAKOLE STREET, WITHIN THE CITY AND REGION OF DODOMA

And

In the matter of an application for Letters of administration by GIVEN ISSAIMANI MINJA

GENERAL CITATION
(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased person are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letter of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 15 day of 1...................... 2025

Dated at Dodoma this 6 day of 12......................2024

RESIDENT MAGISTRATE



KUPOTEA KWA CHETI



**HAPPYNESS AGILAMUNGU DEUSDEDITH,** Anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha Nne chenye Index Namba **S5042-0033** Kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia shule ya Sekondari Mungu Ibariki Mwaka 2020 Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/KAG/KAR/4160/2023**



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WILAYA YA KILOMBERO

MAHAKAMA YA MWANZO MLIMBA

SHAURI LA MIRATHI NAMBA 1/2021

MUOMBAJI....................JOYCE ALEX LYASATO

MAREHEMU ............SILVANUS ALEX LYASATO

MLALAMIKIWA........................VAILETH MHAPA

Kufuatia lalamiko lililoletwa na msimamizi wa Mirathi ya marehemu Silvanus Alex Lyasato dhidi ya Vaileth Mhapa kuhusu pesa zilizotolewa kwenye mfuko wa NSSF. Ndugu Vaieth Mhapa anashauriwa/anaombwa kufika mahakamani siku ya tarehe 12.12.2024 ili kujibu malalamiko hayo. Kutokufika kwake kutailazimu mahakama kusikiliza lalamiko upande mmoja.

HAKIMU MKAZI MWANDAMIZI



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA

MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
KANDA YA MBEYA

SHAURI LA MADAI NAMBA 28290 LA MWAKA 2024

K.W.SECURITY...................................................MDAI

DHIDI YA

EXECUTIVE DIRECTOR TANZANIA NATIONAL ROAD AGENCY NA WENZAKE................................WADAIWA

KWA: A.V.M DILLGHAM CONSTRUCTION
POPOTE ULIPO

KUITWA SHAURINI

Unataarifiwa na Mahakama hii,kuhudhuria hapa Mahakamani binafsi au Wakili wako tarehe 5/02/2025 siku ya Jumatano saa3:00kamili asubuhi bila kukosa ELEWA KWAMBA,Ukikosa kufika siku hiyo,shauri litasikilizwa bila wewe kuwepo na uamuzi utatolewa.
Hati hii imetolewa kwa Mkono wangu na Muhuri wa Mahakama leo hii tarehe 22/11/2024.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA

HABARI KIMATAIFA

# Netanyahu kortini tuhuma za ufisadi

**TEL AVIV,** Israel

WAZIRI Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, amepandishwa kizimbani kujibu tuhuma ya muda mrefu ya madai ya ufisadi, na kwamba makosa mengine yanayomkabili yanahusu kuanzisha tamasha la wiki nzima jambo ambalo linachukuliwa kama hatua ya kuchochea hisia za watu kwa lengo la kufunika masaibu ya kisheria yanayomkabili.

Hayo yanajiri wakati ambako Netanyahu anakabiliwa pia na hati ya kimataifa ya kukamatwa kwake kwa makosa ya uhalifu wa kivita na wakati huo huo mashambulizi ya jeshi la Israel yakiwa yanaendelea katika Ukanda wa Gaza.

**Hatua ya kiongozi huyo kusimama kizimbani kutoa ushahidi inafanyika baada ya Netanyahu na familia yake kukabiliwa kwa miaka mingi ya kashfa hizo.**

Ilielezwa jana kuwa licha ya kiongozi huyo kupandishwa kizimbani lakini awali alijaribu mara kwa mara kuchelewesha kufikishwa kwake mahakamani.

Pia ilielezwa kuwa ni mara ya kwanza kwa waziri mkuu wa Israel kusimamishwa kizimbani akikabiliwa na makosa ya jinai, na kwamba ni hatua ya kufedhehesha kwa kiongozi ambaye mara zote amekuwa akiweka taswira ya kuwa yeye ni mwanasiasa makini, mahiri na kiongozi wa kuheshimika.

Aidha, ilielezwa kuwa Netanyahu atajibu mahakamani mashtaka ya udanganyifu, kuvunja uaminifu na kupokea rushwa katika kesi tatu tofauti zinazomkabili.

Inaelezwa kuwa Netanyahu anatuhumiwa kwa kupokea maelfu ya dola za Kimarekani, sigara na mvinyo wa bei ghali aina ya 'champagne' kutoka kwa bilionea mmoja mtayarishaji wa filamu wa Hollywood kwa makubaliano kwamba angemsaidia katika mambo ya kibinafsi na ya kibiashara.

Pia ilielezwa kuwa Waziri Netanyahu, anakabiliwa na mashtaka yanayohusiana na kuendeleza udhibiti unaonufaisha vyombo vya habari kwa makubaliano kwamba magwiji hao watampa Netanyahu nafasi ya juu kwenye vyombo vya habari pamoja na familia yake.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa Netanyahu alikanusha kufanya makosa hayo, akisema mashtaka hayo ni njama ya kumchafua kisiasa inayoendeshwa na vyombo vya habari vinavyompinga na pia mfumo wa kisheria wenye upendeleo unaolenga kuupindua utawala wake uliodumu kwa muda mrefu.

Hatua ya kiongozi huyo kusimama kizimbani kutoa ushahidi inafanyika baada ya Netanyahu na familia yake kukabiliwa kwa miaka mingi ya kashfa hizo.

Umati wa watu umekusanyika nje ya mahakama ya mjini Tel Aviv, wakiwa ni wafuasi wake na wale wanaompinga Netanyahu, wakiwamo wanafamilia wa mateka wanaoshikiliwa na kwamba Waziri wa Usalama wa Israel, Itamar Ben-Gvir ni miongoni mwa waandamanaji wanaomuunga mkono Benjamin Netanyahu.

Vilevile, ilielezwa kuwa mashtaka dhidi ya Netanyahu yamezusha mgawanyiko mkubwa nchini Israel, huku waandamanaji wakimtaka ajiuzulu na baadhi ya washirika wake wa zamani wa kisiasa wakikataa kuhudumu kwenye serikali ya kiongozi huyo wa Israel na kusababisha mzozo wa kisiasa ambao ndio chanzo cha kufanyika chaguzi tano nchini Israel katika muda wa chini ya miaka minne kuanzia 2019.

Benjamin Netanyahu ndiye waziri mkuu aliyehudumu kwa muda mrefu zaidi katika historia ya Israel, akiwa ameshika wadhifa huo kuanzia mwaka 1996 hadi 1999, kisha mwaka 2009 hadi mwaka 2021, na kuanzia Novemba 2022 na kuendelea hadi sasa. **AFP**

## Ruto, Kenyatta wakutana licha ya uvumi wa kutoelewana

**NAIROBI,** Kenya

RAIS wa Kenya, William Ruto amekutana na mtangulizi wake Uhuru Kenyatta katika kile ambacho wengi wanaita hatua ya kushangaza katika duru za kisiasa za taifa hilo la Afrika Mashariki.


Kenyatta, ambaye alihudumu kama rais kuanzia 2013 hadi 2022, aliunga mkono kugombea urais kwa Waziri Mkuu wa zamani wa Kenya Raila Odinga katika uchaguzi wa Agosti 2022 alishinda kwa kura chache na huku Ruto akiwa naibu wake.

Ilielezwa kuwa Rais Ruto alihudumu kama naibu wa Kenyatta kwa miaka 10, lakini wawili hao walitofautiana wakati wa muhula wa pili wa Kenyatta baada ya mkuu wa nchi wakati huo kufikia makubaliano ya ushirikiano na Odinga, ambaye alikuwa akiongoza upinzani.

Wakati wa kampeni, kuelekea uchaguzi wa Agosti 9, 2022, Kenyatta alisema Rais Ruto hawezi kuaminiwa kuiongoza Kenya kama rais, na kwamba Odinga ndiye chaguo bora zaidi.

Wakati huo huo, Rais Ruto, kwa upande mwingine, alisema utawala wa Kenyatta umefanya kidogo kuboresha maisha ya Wakenya, na kwamba urais wake ndio utang'ara kushinda wa Kenyatta.

Pia ilielezwa kuwa miaka miwili ya uongozi wa Rais Ruto imekuwa ikikabiliwa na maswali kadhaa kuhusiana na hali ya mambo ya Kenya, ikiwa ni pamoja na mpango mpya wa afya wa kitaifa lakini wenye utata, na mtindo wa ufadhili wa elimu ya wanafunzi wa vyuo vikuu.



Rais wa zamani wa Kenya, Uhuru Kenyatta (kushoto), akiwa na Rais William Ruto baada ya kumtembelea kiongozi huyo nyumbani kwake juzi. **PICHA: MTANDAO**

Mengine ni ongezeko la idadi ya watu wanaoripotiwa kutekwa nyara, na kile ambacho Wakenya wanadai ni mchakato wa ununuzi wa neno "opaque" kwenye miradi ya serikali, ambayo ilishuhudia kuporomoka kwa miradi ya viwanja vya ndege na nishati, ambayo ingetekelezwa na Kundi la Adani la India.

Utawala wa Ruto pia umekabiliwa na shutuma za ongezeko la kiholela la ushuru, kushawishi ufisadi na uzembe wa kiutawala kwa ujumla.

Utawala wa Rais Ruto unakanusha vikali madai hayo ambayo pia yametolewa na makundi ya kidini nchini Kenya. **TRT**

## Rais Kiir awatimua gavana, mkuu wa jeshi, polisi

**JUBA,** Sudan Kusini

RAIS wa Sudan Kusini, Salva Kiir amemfuta kazi mkuu wa majeshi ya nchi hiyo, mkuu wa polisi na gavana wa benki kuu licha ya kutobainisha sababu ya maofisa hao kufutwa kazi.

Tangazo lililotolewa usiku wa kuamkia jana kwenye televisheni ya umma lilisema Rais Kiir amemteuwa Paul Nang Majok kuwa mkuu wa majeshi ya ulinzi, akichukua nafasi ya Jenerali Santino Wol.



Ilielezwa kuwa mwishoni mwa mwezi Novemba, jaribio la kumkamata aliyekuwa mkuu wa idara ya ujasusi lilizusha makabiliano ya risasi katika mji mkuu Juba, na kwamba mwezi Oktoba, kiongozi huyo alimtimuwa Akol Koor Kuc, ambaye alikuwa Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa tangu nchi hiyo ilipopata uhuru kutoka kwa Sudan mwaka 2011.

Alielezwa kuwa James Alic Garang alitangazwa kuwa gavana mpya wa benki kuu, na kumrejesha Johnny Damian kwenye wadhifa huo baada ya kumfuta kazi Oktoba 2023. Na kwamba Abraham Peter Manyuat ndiye Inspekta Mkuu wa Polisi akichukua nafasi ya Atem Marol Biar. **DW**

# WASICHANA TANZANIA U-15 WANG'ARA MICHUANO CECAFA

**Na Mwandishi Wetu,** KAMPALA

TIMU ya Soka ya Taifa ya Wasichana wa umri chini ya miaka 15, imeanza vema kampeni ya kusaka tiketi ya kushiriki mashindano ya Shule ya Afrika baada ya kuwachapa wenzao wa Rwanda mabao 5-1.

Katika mechi hiyo iliyoanza kwa kila upande kumsoma mpinzani wake, Tanzania ilienda mapumziko ikiwa mbele kwa mabao 2-0.

Hellena Hamisi alikuwa wa kwanza kupachika bao kwa upande wa Tanzania dakika ya 12 na Bahati Steven akafunga la pili dakika saba baadaye na kumaliza dakika 45 za kipindi cha kwanza wakiwa wanaongoza.

Kipindi cha pili, Hellean alifunga bao la pili na la tatu kwa timu katika mchezo huo huku magoli mengine ya Yosso hao wa Tanzania yakipachikwa na Elizabeth John na Neema Thomas.

**Timu hiyo ya wasichana itashuka tena dimbani leo kuvaana na wenyeji, Uganda na itamaliza michezo yake kesho kwa kuikaribisha Burundi.**

Wakati huo huo, kwa upande wa wavulana, Tanzania ilitoka sare ya bila kufungana dhidi ya Burundi katika mechi iliyochezwa mapema jana asubuhi.

Timu hiyo ya wavulana ilitarajiwa kucheza mechi yake ya pili jana jioni dhidi ya Somalia ambayo mapema asubuhi ilifungwa bao 1-0 na Yosso wa Uganda.

Mashindano hayo yatamalizika kesho kwa kupata timu mbili kila upande (wavulana na wasichana), zitakazokwenda kushiriki michuano ya Afrika (CAF U-15), itakayofanyika baadaye mwakani.

## TUUJAZE UWANJA...



Mashabiki wa Simba wakiwa katika hamasa, kuhamasishana kununua tiketi kuelekea mchezo wao wa Kombe la Shirikisho Afrika Jumapili wiki hii dhidi ya CS Sfaxien ya Tunisia. Jana Simba ilizindua kampeni hiyo ya hamasa Kawe, Dar es Salaam kuelekea mchezo huo. **MPIGAPICHA WETU**



# *Coastal, Matampi waachana akitajwa Singida Big Stars*

**Na Mwandishi Wetu**

IKIWA zimesalia siku nne tu kabla ya kufunguliwa kwa dirisha dogo la usajili Ligi Kuu Tanzania Bara na zingine nchini, Klabu ya Coastal Union imetangaza kuachana na kipa wake namba moja raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Ley Matampi (pichani), huku akihusishwa na Klabu za Singida Black Stars na Dodoma Jiji.

Taarifa iliyotolewa jana mchana na klabu hiyo ilieleza wameachana na kipa huyo kwa makubaliano ya pande zote mbili.

"Tumefikia makubaliano baina ya klabu yetu na golikipa wetu, Ley Ngumbi Matampi ya kumaliza huduma za pande zote mbili. Shukrani za kipekee kwa kocha wetu wa magolikipa Ally Mansour ambaye alitumia nguvu na maarifa makubwa ya kurudisha uwezo na kiwango chako ukawa msaada mkubwa eneo la kulinda lango letu.

"Tunakutakia kheri nyingi, na mafanikio zaidi katika maisha yako," ilisema taarifa hiyo iliyotolewa na Idara ya Habari na Mawasiliano ya klabu hiyo.

Kipa huyo aliyejiunga na timu hiyo Agosti mwaka jana akitokea Klabu ya Jeunesse Sportive Groupe Bazano ya DR Congo, alitangazwa kuwa kipa bora kwa kutwaa tuzo hiyo mwishoni mwa msimu uliopita kutokana na kufanya vema akiwapiga kumbo makipa wengine wakubwa, maarufu na wazoefu kama kina Djigui Diarra wa Yanga na Aishi Manula wa Simba, akiiwezesha Coastal Union baada ya miaka mingi kupata tiketi ya kucheza mechi za kimataifa.

Matampi alikuwa anamaliza mkataba wake mwishoni mwa msimu, lakini mwenyewe amesema umekuwa ni uamuzi sahihi kwake kuondoka kwa wakati huu.

Hata hivyo, zipo taarifa kuwa kuna baadhi ya klabu za hapa hapa zinamhitaji hasa Singida Black Stars na Dodoma Jiji, lakini zipo nyingine pia nje ya nchi zinazohitaji huduma yake, hivyo huenda asiondoke nchini badala yake kuibukia kwenye timu nyingine kipindi cha usajili wa dirisha dogo.

# Kocha Yanga Princess sasa aanza tambo

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupata ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Mlandizi Queens juzi kwenye Uwanja wa KMC Complex, Mwenge, Dar es Salaam, Kocha Mkuu wa timu ya soka ya wanawake, Yanga Princess, Edna Lema, ametamba kuwa sasa ndiyo wameanza ligi.

Lema, amesema ushindi walioupata juzi, ukiwa ni wa pili mfululizo kwao, unaonesha kuwa vijana wake wameimarika, hivyo sasa wanaweza kushinda mechi nyingi zijazo baada ya kuwa na wakati mbaya mwanzoni mwa ligi hiyo.

"Tunashukuru tumeshinda mchezo wa pili kwenye Ligi Kuu, hatukuwa kwenye nyakati nzuri, yaani hapa ndiyo kwanza sasa tunaanza ligi, tulipoteza pointi tisa kwenye michezo minne, tukaenda kushinda ugenini dhidi ya Fountain Gate na leo tumeshinda hapa unaona kabisa timu inazidi kuimarika siku hadi siku.

"Mara nyingi timu ikishinda ina maana wachezaji wanazidi kujiamini kuelekea michezo ijayo, siwezi kusema ndiyo tumefika juu kabisa ya ubora na kufanya kile tunachokitaka, lakini maendeleo yetu sasa ni mazuri," alisema kocha huyo.

Baada ya kucheza mechi nne za mwanzo, ikitoa sare tatu na kupoteza moja, Yanga Princess hatimaye ilipata ushindi wa kwanza kwenye Ligi Kuu, Novemba 19, mwaka huu, ikiifunga Fountain Princess mabao 2-1, kabla ya juzi kupata ushindi wa pili kwenye raundi ya sita dhidi ya Mlandizi Queens.

Yalikuwa ni mabao mawili ya Neema Paul, Asha Omary na Neema Shau, ushindi ambao umeipandisha hadi nafasi ya tatu ikifikisha pointi tisa, lakini itaendelea kukaa hapo kutegemea na mechi zingine zilizotarajiwa kucheza jana jioni.

Kipigo cha mabao 4-0 ilichokipata juzi, kinaibakisha Mlandizi Queens mkiani ikiwa na pointi moja, ikicheza mechi sita, haijashinda mchezo wowote, sare moja na kupoteza mitano.



HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### PALMER AIVUTIA MADRID

MSHAMBULIAJI wa England, Cole Palmer mwenye umri wa miaka 22, anaivutia Real Madrid kwa sababu ya mchezo wake bora akiwa Chelsea. ***(Fichajes)***

### FERGUSON ATAJWA WEST HAM

KLABU ya West Ham itaongeza nia ya kutaka kumnunua mshambuliaji wa Brighton na Jamhuri ya Ireland, Evan Ferguson mwenye umri wa miaka 20, wakati wa dirisha la uhamisho la Januari litakapofunguliwa. ***(Football Insider)***

### ARSENAL, BARCA KWA DAVID

ARSENAL, Manchester United na Barcelona wako tayari kupigana vikumbo kwa ajili ya kumnasa fowadi wa Lille kutoka Canada, Jonathan David mwenye umri wa miaka 24, ambaye mkataba wake unamalizika msimu wa majira ya joto. ***(Mundo Deportivo)***

### CITY WAKOMAA NA WIRTZ

KLABU ya Manchester City iko tayari kumuuza mshambuliaji wa Norway, Oscar Bobb mwenye umri wa miaka 21, au kiungo wa kati wa England, James McAtee (22), huku wakitafuta kuwashawishi Bayer Leverkusen kumwachia winga wao wa miaka 21 raia wa Ujerumani, Florian Wirtz. ***(TBR Football)***

### AMORIM KUMUUZA ERIKSEN

KOCHA wa Manchester United, Ruben Amorim anaweza kuwatoa kiungo wa kati wa Denmark, Christian Eriksen mwenye umri wa miaka 32 na winga wa Brazil, Antony mwenye miaka 24, ili kuokoa fedha Januari. ***(GiveMeSport)***

### LIVERPOOL YASAKA NYOTA

LIVERPOOL inatumaini kuwashinda wapinzani kadhaa wa Ulaya katika mbio za kuinasa saini ya beki wa Bologna, Sam Beukema, 26. ***(Teamtalk)***

### MILLER ATAKIWA ANFIELD

KIUNGO wa kati wa Motherwell na Scotland, Lennon Miller mwenye umri wa miaka 18, pia analengwa na Liverpool na anaweza kupatikana kwa pauni milioni 8. ***(Caught Offside)***

### BETO KURUDI ITALIA

BETO wa Everton mwenye umri wa miaka 26, anaweza kurejea Italia Januari, huku Torino ikimtaka mshambuliaji huyo wa Guinea-Bissau. ***(Tuttomercatoweb)***

### LOOKMAN AWANIWA EPL

MCHEZAJI wa Atalanta, Ademola Lookman mwenye miaka 27, yuko tayari kurejea England, huku klabu kadhaa za Ligi Kuu ya England zikimtaka fowadi huyo wa Nigeria. ***(GiveMeSport)***

### KELLYMAN KWA MKOPO

CHELSEA itampeleka kiungo wa kati wa England, Omari Kellyman, kwa mkopo dirisha la Januari ili kumsaidia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19, kupata uzoefu wa juu. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SALIBA HANA MPANGO WA KUTUA REAL MADRID

**LONDON,** England

MLINZI wa Arsenal, William Saliba, ameahidi kwamba ana mustakabali wa muda mrefu katika klabu hiyo huku kukiwa na tetesi zinazomhusisha na Real Madrid.

**Saliba ameibuka kuwa mmoja kati ya mabeki bora wa kati katika soka la dunia misimu ya hivi karibuni, huku Madrid wakishuhudia safu yao ya ulinzi ikikabiliwa na majeraha.**

Oktoba, beki wa kati wa sasa wa Madrid, Antonio Rudiger alimtaja Saliba kama mtu anayetaka kucheza naye pale katika dimba la Bernabeu.

Lakini Saliba anaonekana ana mawazo mengine.

Alipoulizwa kuhusu mustakabali wake katika siku zijazo, Saliba alifichua kuwa hana nia ya kuondoka Arsenal, ambapo mkataba wake utaendelea kwa misimu mingine miwili baada ya mwaka huu.

"Nilisajiliwa na klabu miaka mitano iliyopita, lakini huu ni msimu wangu wa tatu pekee," alisema Saliba mwenye umri wa miaka 23.

"Ninafurahia kila kitu - wachezaji, wafanyakazi na mashabiki. Ninahisi niko nyumbani kwa hiyo bila shaka ninaweza kukaa kwa muda mrefu hapa."

> Ninafurahia kila kitu hapa, ninahisi niko nyumbani hivyo ninaweza kukaa muda mrefu...

Mfaransa huyo alijiunga miezi michache tu baada ya siku yake ya kuzaliwa ya kutimiza umri wa miaka 18 katika majira ya joto ya mwaka 2019 kwa mkataba wa thamani ya pauni milioni 27.

Iliibua sintofahamu kwa sababu alikuwa na kipaji kisichojulikana baada ya mechi 19 pekee za kikosi cha kwanza akiwa na Saint-Etienne.

Saliba alitangazwa kuwa mchezaji bora chipukizi wa mwaka wa Ligue 1 na alijumuishwa tena kwenye kikosi cha kwanza cha Arsenal na Mikel Arteta kabla ya msimu wa 2022/23.

## HABARI MICHEZO

# MESSI, RONALDO NJE FIFPRO XI



**LIVERPOOL,** England

KYLIAN Mbappe amejumuishwa katika kikosi cha wachezaji 11 bora cha mwaka cha Dunia 2024 (FIFPro XI) pamoja na wachezaji watano wa Ligi Kuu England, huku Lionel Messi, Cristiano Ronaldo na Mohamed Salah wakitoswa.

Mbappe ambaye amekuwa na mwanzo mgumu msimu huu amejumuishwa na Vinicius Junior ambapo ni wachezaji wawili kati ya sita walioichezea Real Madrid katika mwaka wa kalenda, pamoja na Erling Haaland wa Manchester City.

Haaland anaungana na wachezaji wenzake Kevin De Bruyne, Ederson na mshindi wa Ballon d'Or, Rodri katika kwenye kikosi hicho, ambapo kura hupigwa na wachezaji. Pia nahodha wa Liverpool, Virgil van Dijk naye amejumuishwa kwenye kikosi hicho.

Messi nahodha wa Argentina na Inter Miami amekosekana kwenye kikosi hicho kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2006.Messi, mchezaji aliyepambwa zaidi katika soka, alikuwa amefanikiwa kuingia kwenye kikosi hicho mara 17 mfululizo, lakini amekosekana mwaka huu wa 2024.

Mpinzani wake wa muda mrefu, Ronaldo, ambaye aliingia kwenye timu hiyo mara 16 kabla ya 2023, pia amekosekana sawa na Salah licha ya kiwango chake cha mabao akiwa na Liverpool.

Kiungo wa kati wa England na Real Madrid, Jude Bellingham, amejumuishwa pamoja na wachezaji wenzake wa zamani na wa sasa Antonio Rudiger, Dani Carvajal, na Toni Kroos, ambaye alistaafu baada ya kuichezea Ujerumani kwenye Euro 2024 msimu wa majira ya joto.

# Sancho kuwanyamazisha waliomkosoa




**MANCHESTER,** England

WINGA wa Chelsea, Jadon Sancho, amesema kwamba msimu huu ana nafasi ya kuwathibitishia ubora wake watu wengi waliomkosoa kuhusu kiwango chake alipokuwa akipitia wakati mgumu pale Manchester United.

Sancho alijidhihirisha kama mmoja wa vipaji bora barani Ulaya wakati wa miaka yake minne kule Borussia Dortmund, na kupata uhamisho wa pauni milioni 73 kwenda Old Trafford wakati akiwa na umri wa miaka 21 tu.

Winga huyo alikuwa na wakati mgumu pale United baada ya kupata maambukizi ya sikio wakati wa maandalizi ya msimu mpya.

Mwaka wake wa pili ulianza vizuri vya kutosha kabla ya "mchanganyiko wa masuala ya kimwili, lakini pia kiakili", kama ilivyofichuliwa na Erik ten Hag wakati huo, na kusababisha kuachana na timu hiyo.

Malumbano ya hadharani na kocha Ten Hag yalishuhudiwa na mchezaji huyo akifukuzwa mwaka 2023 na kurudishwa kwa mkopo Dortmund.

Sancho alionesha kiwango kizuri akiwa Ujerumani akielekea fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, hasa katika nusu fainali dhidi ya Paris Saint-Germain, akifungua milango ya uwezekano wa kurudishwa Manchester.

Alionekana kama mchezaji wa akiba kwenye Ngao ya Jamii, lakini aliachwa katika vikosi vilivyofuata vya Ligi Kuu kutokana na kile kilichoripotiwa kuwa ugonjwa mwingine wa sikio. Mkopo wa kwenda Chelsea na ofa ya kumsajili kwa moja kwa moja ulifuatiwa.

"Kuanzia siku ya kwanza, walinifanya nijisikie nimekaribishwa Chelsea," alisema Sancho mwenye umri wa miaka 24, akiiambia SuperSport.

"Najua kwamba nina watu wengi wa kuwathibitishia ubora wangu. Nimekuwa nikifanya kazi kwa bidii sana. Niseme asante kwa wafanyakazi na timu kwa kuniamini na kunipa nafasi hii."

# Allister: Awataka Arnold, Van Dijk kubaki Liverpool

**LIVERPOOL,** England

ALEXIS Mac Allister ana matumaini mchezaji mwenzake wa Liverpool, Trent Alexander-Arnold ataendelea kubakia katika klabu hiyo msimu ujao.

Vile vile kwa nahodha, Virgil van Dijk na fowadi Mohamed Salah, ambao wamekuwa kwenye mazungumzo ya kuongeza mikataba mipya wakati ile ya sasa ikingia kwenye miezi sita ya mwisho.

Alexander-Arnold amekuwa akihusishwa na Real Madrid, lakini sasa beki huyo wa kulia wa England yuko kwenye mazungumzo ya kusaini mkataba mpya wa kubaki hapo Anfield.

"Natumaini Trent na Virgil wanaweza kuendelea na sisi pamoja na Salah," alisema Mac Allister akiiambia Diario AS.

"Alexander-Arnold ni mchezaji muhimu kama tulivyoona dhidi ya Manchester City aliporejea kutoka kwenye chumba cha majeruhi.

"Kama Salah, yuko kwenye mazungumzo na tunatumaini anaweza kuendelea kwenye timu hii."

"Ubora wake ni mkubwa," aliongeza Mac Allister kuhusu nyota huyo wa kimataifa wa England.

"Siku zote nimekuwa nikisema kwamba alikosolewa kwa nafasi yake ya ulinzi, lakini sina shaka kwamba katika safu ya ulinzi na ushambuliaji ni mchezaji wa tofauti. Pia ni mwenye nguvu na mwepesi ambapo unamwezesha kupata uwiano huo kati ya mashambulizi na ulinzi."



# HABARI MICHEZO

## Fadlu awapania Watunisia, watua

INATOKA UK. 24

ushindani wa namba kikosini, huku wachezaji kama Augustine Okejepha na Fabrice Ngoma wakionesha kiwango kizuri kwa siku za karibuni, hivyo hakuona vibaya kuwatumia na kumpumzisha Mavambo ili aingie kipindi cha pili.

"Okejepha yupo kwenye kiwango cha juu, Ngoma pia, hii ni nzuri kwenye kuleta ushindani na kuwania namba, ndiyo maana nilimweka nje ili aje kusaidia kipindi cha pili, ukweli kila kitu kilikwenda sahihi, ni makosa tu yaliyojitokeza tukaruhusu mabao rahisi ndiyo yaliyoharibu kila kitu," alisema Fadlu.

Wakati huo huo, wapinzani wa Simba, CS Sfaxien, walitua nchini jana wakitokea nchini Angola ambako Jumapili iliyopita walicheza mchezo wa Kombe la Shirikisho Kundi A, na kuchapwa mabao 3-2 dhidi ya Bravo do Maquis ya nchini humo.

CS Sfaxien imetua mapema, ambapo taarifa zinaeleza sababu za kijiografia ndizo zimesababisha kuwasili mapema, kwani isingewezekana kutoka Angola kurudi Tunisia na kuja nchini, huku zingine zikieleza wamewahi kwa ajili ya kuzoea hali ya hewa ya Dar es Salaam ambayo ni joto, kabla ya mchezo wao wa Jumapili dhidi ya Simba.

Katika hatua nyingine, uongozi wa klabu hiyo umetangaza viingilio vya mchezo huo kuwa ni Sh. 3,000 kwa mzunguko, Sh. 5,000 rangi ya machungwa, Sh. 10,000 VIP C, Sh. 20,000 VIP B, Sh. 30,000 VIP A na Sh. 150,000 kwa upande wa Platinum huku Tanzanite ikiwa ni Sh. 200,000.

## Yanga: Tutakufa na TP Mazembe

INATOKA UK. 24

kwa mabao 2-0, lakini safari bado inaendelea pamoja na kwamba kundi ni gumu kwani tumepoteza michezo miwili, ila haijaisha mpaka iishe, tunajiandaa siku mbili hizi, tutaelekea Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo katika mchezo wetu wa tatu, bahati nzuri wachezaji wetu wote majeruhi wameshapona, kasoro Shadrack Boka ndiyo hatutakuwa naye katika mchezo ujao," alisema Ngai.

Baada ya kufungwa mabao 2-0 katika michezo miwili mfululizo dhidi ya Al Hilal Omdurman ya Sudan, Yanga inaburuza mkia kwenye Kundi A ikiwa haina pointi wala bao, TP Mazembe ikiwa na pointi moja kwenye nafasi ya tatu, MC Alger ina pointi nne, ikiwa nafasi ya pili na Al Hilal ikiongoza kundi kwa kukusanya pointi sita hadi sasa.

# WASANII WAING'ARISHA DAR TAMASHA BATA LA DESEMBA

**Na Mwandishi Wetu**

TAMASHA lililosubiriwa kwa hamu kubwa, Bata la Desemba, lililofanyika kuanzia Desemba 6 hadi 8, mwaka huu, katika viwanja vya Leaders Club, limehitimishwa kwa mafanikio makubwa likiwa na sherehe za kusisimua za muziki, utamaduni na mshikamano wa jamii.

Kwa ujumla tamasha hilo lilihusisha maonesho ya wasanii wakubwa wa Afrika, wakiwamo Zuchu, Master KG, Chino Kidd, Linah Sanga, Johmakini, G Nako, na wengine wengi ambapo watazamaji walifurahia mchanganyiko wa muziki, michezo, ucheshi na matangazo mubashara ya michezo, ambayo yaliendelea kuweka hewa ya shangwe kwa siku zote tatu.

Mbali na burudani, tamasha hilo pia lilitoa fursa kwa wachuuzi wa ndani, likionesha utofauti wa vyakula vya Dar es Salaam na kuwapa wajasiriamali wa ndani nafasi ya kuwasiliana na maelfu ya wateja watarajiwa, hiyo ikiendana na lengo pana la kusaidia uchumi wa ndani na kuunda fursa za ukuaji.

**Tukio hili, lililoandaliwa na Heineken Beverages International kwa ushirikiano na Mkoa wa Dar es Salaam, limekusanya zaidi ya watu 3,000 kwa siku tatu za burudani ya kiwango cha juu, vyakula vya asili, michezo mubashara, na onesho la wasanii la kuvutia.**

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, hakusita kuelekezea fahari yake kwa mafanikio ya tamasha hilo.


"Tamasha la Bata la Desemba halikuonesha tu nishati ya kipekee ya Dar es Salaam bali pia liliangazia jiji letu kama kitovu cha utamaduni, biashara, na ukuaji wa uchumi. Tukio hili limeonesha umaarufu wa Dar es Salaam kama kitovu cha utalii na utamaduni huku tukisherehekea mshikamano na furaha inayotutambulisha kama jamii," alisema.

Obabiyi Fagade, Meneja wa Nchi (country manager) wa Heineken Beverages International nchini Tanzania, alisema: "Mafanikio ya Bata la Desemba ni kielelezo halisi cha maadili tunayoyasimamia - kuwaleta watu pamoja kusherehekea, kuleta furaha, na kuchangia ustawi wa kiuchumi wa jamii ya hapa.

"Tukio hili halikutoa tu jukwaa la burudani ya kiwango cha dunia bali pia liliwaunga mkono wafanyabiashara wa ndani na wajasiriamali, likichangia ukuaji wa uchumi wa Tanzania."

Alisema katika kipindi chote cha tamasha, walionesha dhamira yao ya kukuza mshikamano na kushirikiana na kwamba tukio hilo halikuwa tu nafasi kwa Watanzania na wageni wa kimataifa kuungana, bali pia lilionesha uwezo wa kanda hii kama kiungo muhimu katika mazingira ya kiuchumi ya Afrika Mashariki.

Tamasha hilo lilimalizika kwa onyesho la fataki kusherehekea miaka 63 ya uhuru wa Tanzania ambapo washiriki walionesha furaha yao na shukrani kwa mazingira mazuri na utekelezaji mzuri wa tukio hilo. Wengi walilitaja kama tukio kubwa na la kukumbukwa zaidi kwa mwaka huu, huku mchanganyiko wa burudani, utamaduni, na mshikamano ukiacha athari kubwa kwa wote walioshiriki



Zuchu akipagawisha jukwaani jijini Dar es Salaam katika Tamasha la Bata la Desemba, wiki iliyopita. **MPIGAPICHA WETU**

## Kagera, Namungo uso kwa uso Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya siku nne za mapumziko, Ligi Kuu Tanzania Bara itaendelea leo kwenye viwanja viwili nchini.

JKT Tanzania itakuwa kwenye uwanja wake wa nyumbani, Meja Jenerali Isamuhyo kucheza dhidi ya Pamba Jiji saa 10:00 jioni, huku saa 1:00 usiku katika Uwanja wa Kaitaba, Bukoba, mkoani Kagera, wenyeji, Kagera Sugar wataikaribisha Namungo FC.

Kocha Mkuu wa JKT Tanzania, Ahmad Ally, amesema wachezaji wake wako tayari kwa mchezo huo huku benchi la ufundi likiwa limemaliza kazi.

"Sisi kwa upande wetu tumemaliza, kazi iliyobaki ni kwa wachezaji wenyewe kutupa kitu ambacho tumewaambia watuonyeshe uwanjani," alisema kocha huyo.

JKT Tanzania inakwenda kucheza mechi hiyo ikiwa ni siku tatu tu tangu ilipoibamiza Igunda FC mabao 5-1 katika mchezo wa raundi ya tatu ya Kombe la FA.

Timu hiyo inayoshika nafasi ya nane kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi 16 kwa mechi 11 ilizocheza, imeshinda michezo yake yote miwili iliyocheza hivi karibuni kwa bao 1-0, dhidi ya Prisons na Fountain Gate ilizozicheza baada ya siku 29 za kukaa nje ya dimba kutokana na wachezaji wake kupata ajali.

Hali ni tofauti na wapinzani wao Pamba Jiji ambao wapo nafasi ya 13 ya msimamo, ikicheza mechi 13, ikiwa na pointi 11. Kwenye Uwanja wa Kaitaba itazikutanisha timu ambazo hazifanyi vizuri sana kwenye Ligi Kuu msimu huu, huku zikifuatana kwenye msimamo.

Kagera Sugar inashika nafasi ya 14, ikiwa imecheza michezo 13, ikishinda miwili, sare tano, ikipoteza tano na pointi zake 10, huku Namungo ikiwa nafasi ya 15, ikicheza mechi 12, ikishinda tatu, haijatoka sare, ikipoteza michezo tisa, ikiwa na pointi tisa.

Kagera Sugar haijashinda mechi tatu mfululizo za Ligi Kuu tangu ilipoifunga Dodoma Jiji mabao 2-1, Novemba 4, mwaka huu, ikitoka suluhu dhidi ya Prisons, bao 1-1 dhidi ya Mashujaa, ilichapwa pia bao 1-0 dhidi ya Azam FC.

Namungo nayo tangu ilipoifunga Pamba Jiji bao 1-0, Oktoba 28, mwaka huu, ilipoteza mechi zake zote tatu zilizofuata, ikifungwa bao 1-0 dhidi ya KMC, Mashujaa kwa idadi kama hiyo, na mabao 2-0 dhidi ya Yanga.

# Michezo

Jumatano Desemba 11, 2024

Nipashe




Messi, Ronaldo nje FIFPro XI UKURASA 22

TUTAWASHIKA...



Kiungo mshambuliaji wa Yanga, Pacome Zouzoua, akiwa mazoezini na wenzake katika viwanja vya TRA, Dar es Salaam jana, wakijiandaa na mchezo wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya TP Mazembe ya DR Congo utakaopigwa nchini humo Jumamosi wiki hii. **MPIGAPICHA WETU**

## Fadlu awapania Watunisia, watua

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amewaahidi wanachama na mashabiki wa timu hiyo ushindi Jumapili dhidi ya CS Sfaxien ya Tunisia utakaochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, huku wapinzani wao hao wakiwasili nchini mapema tayari kwa mchezo huo.

Akizungumza jana alfajiri wakati kikosi cha timu hiyo kikiwasili nchini kutoka Algeria kilipocheza mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya CS Constantine katika Uwanja wa Mohamed Hamlaoui na kufungwa mabao 2-1 Jumapili iliyopita, kocha huyo alisema anawaahidi wanachama na mashabiki wa Simba si ushindi tu peke yake bali na soka safi.

"Nawaahidi wanachama na mashabiki wa Simba ushindi na soka safi, waje kwa wingi Benjamin Mkapa Jumapili, najua wakijaa pale uwanjani huwapa hamasa wachezaji kufanya vizuri, mechi tuliyopoteza ugenini mmeona hata ninyi tumepoteza kwa bahati mbaya, lakini tunaahidi kufanya vema mchezo ujao," alisema kocha huyo.

Akizungumzia mechi iliyopita na makosa yaliyofanywa na mabeki wa timu yake, alisema binadamu hujifunza kutokana na makosa, na anadhani wachezaji wake wameshaona madhara na hawatakiwi kuyafanya tena.

"Tulikuwa na kiwango kizuri kwa kipindi chote cha dakika 45, hatukuwa vema dakika tano za kwanza kipindi cha pili, tukaruhusu mabao yaliyoamua mchezo, lakini baada ya hapo, tulirejea mchezoni, imetuhuzunisha sana kupoteza mchezo, ila imetufunza kuwa kwenye michezo ya kimataifa makosa madogo madogo, yanaweza kusababisha madhara, hivyo hatutakiwi kuyafanya, na sisi inabidi tuyatumie kama wapinzani wetu wakiyafanya.

"Kwa bahati nzuri tuna mchezo mwingine nyumbani dhidi ya CS Sfaxien ya Tunisia, tunaweza kusawazisha makosa yote kwenye mchezo huo," alisema kocha huyo.

Kocha huyo alisema sababu ya kumweka nje, Debora Fernandes Mavambo, kwenye mchezo huo na kumuingiza kipindi cha pili, ni kutokana na

INAENDELEA UKURASA 23

# Yanga: Tutakufa na TP Mazembe

**Na Adam Fungamwango**

### ●●● Yasema inachotaka ni ushindi tu huku ikitamba majembe yao majeruhi kuwa kamili, hivyo...

HUKU ikitarajia kuelekea DR Congo keshokutwa, Alhamisi tayari kwa mchezo wao wa Kundi A Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya TP Mazembe, Mkurugenzi wa Ufundi wa Klabu ya Yanga, Abduhamid Moallin, amesema kwa sasa wamesahau kila kitu kilichotokea nchini Algeria, badala yake wanaelekeza nguvu kwenye mechi hiyo itakayopigwa Jumamosi katika uwanja wa klabu hiyo mjini Lubumbashi.

Mkurugenzi huyo amewataka wanachama na mashabiki kusahau yaliyopita, badala yake kuisapoti timu ili kwenda kupata ushindi ugenini utakaowarudisha kwenye reli ya kujaribu kucheza robo fainali ya pili mfululizo ya Ligi ya Mabingwa Afrika kama ilivyokuwa msimu uliopita.

Akizungumza juzi jioni, Moallin, ambaye ana taaluma ya ukocha, alisema kipigo walichokipata cha mabao 2-0 kwenye Uwanja wa Julai 5, Algiers nchini Algeria, dhidi ya MC Alger, Jumamosi iliyopita, kilichangiwa na vitu mbalimbali, ikiwamo kikosi kukumbwa na majeruhi, pamoja na hali ya hewa.

"Tuna muda mfupi sana wa kujiandaa kwa mazoezi na safari, lakini tutaanza mazoezi haraka kwa ajili ya mchezo dhidi ya TP Mazembe, mchezo ulikuwa mgumu, tuliweka nguvu zote, wachezaji walicheza kwa juhudi zao zote, lakini vitu vingi vimechangia, hali ya hewa haikuwa rafiki kwetu, kwa sasa tunasahau hilo tunajiandaa na mechi ijayo, ni muhimu sana kwetu kwani inashikilia mustakabali wetu.

> **"Tunatakiwa tushinde ili kurudi kwenye mstari, hivyo ni lazima tukacheze kama fainali," alisema kocha huyo wa zamani wa KMC na Azam FC.**

Naye Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Yanga, Alex Ngai, ambaye aliambatana na kikosi hicho, alisema jijini Dar es Salaam kuwa kilichowagharimu ni idadi kubwa ya majeruhi waliokuwa nao, lakini akiahidi kuwa hawajakata tamaa na safari bado inaendelea.

"Ilikuwa ni mechi ngumu, mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, kingine kilichotugharimu ni idadi ya majeruhi, tumepoteza

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >